القرآن الحكيم

QURANI TAKATIFU

Swahili Quran Translation

INTRODUCTION - UTANGULIZI

by
Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy
(Former Chief Kadhi of
Zanzibar and Kenya)

YALIYOMO

MAELEZO YA MTANGAZAJI.. i

DIBAJI.. v

PONGEZI.. ix

MSINGI WA KUFAHAMU QURANI...................................... xi

FAHARISI YA SURA... xxix

FAHARISI YA JUZUU.. xxxii

MAELEZO JUU YA CHAPA YA TANO

Bismillahir-Rahmanir-Rahym

Alhamdulillah! Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuendelea kukihudumia Kitabu Chake kitukufu. Na sasa, kwa furaha kubwa na shukrani za dhati kwa Allah (s.w.), tunawaletea wasomaji wetu watukufu chapa ya tano ya Qurani Takatifu zikiwa nakala 20,000. Kabla ya kuipeleka hii chapa ya tano mtamboni, tuliupitia upya Msahafu wote, na tukasahihisha makosa tuliyoyagundua.

Sifa njema, utukufu na uwezo wote ni wa Allah (s.w.) aliyetuwezesha kutoa hii chapa ya tano.

THE ISLAMIC FOUNDATION,
P.O. Box 30611,
Nairobi, Kenya.
27th Dhul-Hijjah, 1407 (21st August, 1987)

DR. MOHAMMED SAYIED,
Katibu Mkuu.

MAELEZO YA MTANGAZAJI

Bismillahir-Rahmanir-Rahym.

Amejaalia Mwenyezi Mungu Mtukufu Kitabu Chake Kitukufu hiki kiwe ndicho cha ujumbe wa mwisho unaotoka mbinguni. Na amekiteremsha kwa huyu Mtume wa Mwisho mbora wa Mitume wake — Nabii Muhammad — Muongozi wa viumbe wote.

Na Mwenyezi Mungu alileta Mitume Ambiyaa na Mitume Mursalina kwa watu wote, baada ya kila muda, katika nchi mbali mbali; kama Mitume Mursalina hawa: Adamu, Nuhu, Ibrahimu, Ismaili, Is-haqi, Yaaqubu, Yusufu, Musa, Daud, Suleiman, Yahya, Isa.

Na wengine akawateremshia Vitabu Vyake. Na ilivyokuwa Vitabu hivi wameteremshiwa uma makhsusi na nyakati makhsusi basi havikusalimika — mwishowe — na miongezo na migeuzo na mipachiko.

Na hivyo vitabu wanavyodai baadhi ya watu kuwa ni vya Mungu vimeteremka mbinguni — hawawezi watu hao kuonesha kwa yakini na uhakika zipi humo hizo sehemu za asli zilizoteremka mbinguni na hizo zilizoongezewa baadaye katika zama mbali mbali.

Na ilivyokuwa Vitabu hivyo Mwenyezi Mungu kaviteremsha kwa haja za nyakati makhsusi tu ndiyo maana asivihifadhi na kupotea. Ama Qurani tukufu ameiteremsha juu ya Mtume wa mwisho ambaye hakuletwa baada yake Mtume Nabii wala Mtume Mursali. Wala hataletwa. Na akakamilisha kwa Kitabu hiki kitukufu dini yake ya haki na akatimiza kwa Kitabu hiki neema yake juu ya watu wote na akakijaalia Uwongozi na Mwangaza mpaka siku ya Kiama.

Si haya tu basi, bali akaahidi kuwa atakihifadhi Kitabu Chake hiki — Qurani — hakitapunguzwa, hakitaongezwa na HAITAWEZEKANA kupingwa wala kuonekana na makosa, la kwa vitabu vilivyotangulia.

Na huu Msahafu tulionao uliotapakaa ulimwengu mzima, tunaweza kusema — bila ya shaka yoyote wala kusitasita — kuwa haya ndiyo nafsi ya maneno aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu Subhanahuu Wataala kwa Mtume Wake Muhammad *Salla Ilahu Alyhi W'aalihy Wasallam* kwa karne kumi na nne na zaidi tangu leo. Basi kama alivyoahidi kukihifadhi na kukichunga Kitabu Chake hiki basi kitasalia kama kilivyo mpaka kije Kiama na ulimwengu umalizike. Katika Aya 9 ya *Suratul Hijr* Mwenyezi Mungu amesema:

"Hakika sisi ndio tulioteremsha mauidha haya (hii Qurani); na hakika SISI NDIO TUTAKAOYALINDA."

Na kwa bahati mbaya umekuwa Uislamu sasa unaitakidiwa ni dini ya watu makhsusi — wenyewe Waislamu. Kwa hivyo inaitakidiwa Qurani kuwa ni Kitabu Kitakatifu cha Waislamu na inaitakidiwa Nabii Muhammad ni Mtume wa Waislamu peke yao na Muongozi wao peke yao.

Kuleta fikra hii na kuitangaza kunatokana na wasiokuwa Waislamu ima kwa madai yao tu juu ya dini hii au kwa uchache wa kujua kwao. Mwenyezi Mungu Amesema katika Kitabu Chake cha mwisho kuwa Muhammad s.a.w. alikuwa si kama Mitume waliotangulia kwa sababu ni yeye tu aliyeletwa kwa wanaadamu wote, na kabila zote, na rangi zote, na mataifa yote. Katika Aya ya 158 ya *Al-Aaraf,* Mwenyezi Mungu amesema:

"Sema (Ewe Nabii Muhammad): "Enyi watu! Hakika mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenu nyinyi nyote; (Mungu) ambaye anao ufalme wa mbingu na ardhi, hapana aabudiwaye (kwa haki) ila yeye; yeye ndiye ahuishaye na ndiye afishaye. Basi Mwaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, aliye Nabii Ummy (asiyejua kusoma wala kuandika), am-

baye humwamini Mwenyezi Mungu na maneno yake. Na mfuateni yeye ili mpate kuongoka."

Na hakika wenyewe Waislamu wameregea katika kutekeleza wajibu wao wa kusimamisha shahada hii ya haki kwa watu wote. Yawapasa Waislamu wote kutangaza Uislamu wa kweli kwa wanaadamu wote. Haukuwa Uislamu kwa ajili ya watu maalumu wala ukoo maalumu. Uislamu ni muangaza wenye uwongozi wa kiroho na kimaisha kwa wanaadamu wote. Sasa imebaki kwa wale watakao kujua haki waitafute kwa kusoma Qurani na kwa kufahamu yaliyomo ndani yake.

Kwani Qurani ni atiya ya kiroho waliopewa wanaadamu wote na Mwenyezi Mungu, wawe shirika sawa sawa. Na Qurani imesemeza watu wote; haisemezi watu makhsusi. Wala haihusu uma makhsusi na kuufadhilisha kuliko uma mwengine, wala haiwainui hawa ikawadidimiza wale. Qurani na Risala ya Mwenyezi Mungu kwa wanaadamu wote ili iwape SAADA wanaadamu wote daima milele.

Ujumbe wa Mwenyezi Mungu huu unasadikisha yote aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu juu ya Ambiyaa wote na Mursalina wote tangu Nabii Adamu mpaka Nabii Isa bin Maryamu na unakamilisha ujumbe wao. Basi ujumbe wa Mwenyezi Mungu umekamilika kwa hiki Kitabu cha MWISHO na Mtume wa MWISHO.

Na Waarabu walikuwa ndio watu wa mwanzo aliowasemesha; basi ikateremka Qurani kwa lugha ya Kiarabu; khalafu ifasiriwe kwa lugha nyengine zote. Akaambiwa kila mmoja katika Waislamu apanie barabara kuufikisha huu ulingano wa haki kwa watu wote wa ulimwengu wote.

Na tarekhe zinashuhudia kuwa Waislamu waliutekeleza wajibu huu kama inavyopasa na wakafikisha ujumbe wa Mwenyezi Mungu katika kila pembe miongozi mwa pembe za ulimwengu. Wakayafasiri maana ya maneno ya Qurani kwa lugha zote za ulimwengu zilizokuwa zikijulikana zama hizo ili wapate faida ya yaliyomo katika Qurani wale wasiojuwa lugha ya Kiarabu; wafuate hukumu zake na amri zake na wajiepushe na makatazo yake hata wafinyangike kwa sura inayopenda Uislamu wafinyangike.

Na katika lugha zilizo muhimu kabisa zinazotumika Mashariki ya Afrika ni lugha ya Kiswahili inayosemwa na mamilioni ya watu huku. Na kwa bahati mbaya nchi hizi hazikupata bahati ya kupata tafsiri ya Qurani ya kweli ya kutegemewa mpaka ikatangazwa chapa ya kwanza ya Qurani Takatifu.

Na kwa bahati nzuri chama cha Islamic Foundation cha Nairobi kimepata kwa mara ya tatu bahati hii ya kutowa hii tafsiri ya Qurani ya haki na ya kutegemewa. Na hii ni fadhila ya Mwenyezi Mungu anayompa anayemtaka.

Na hii tafsiri ya Qurani wanayoitoa Islamic Foundation kuwapa Waislamu wote ameifasiri mmoja wa wale wanavyuoni wakubwa wanaojulikana mno Mashariki ya Afrika nzima. Naye ni Sheikh Abdulla Saleh Farsy aliyekuwa Kadhi wa Zanzibar zamani; na leo ni Kadhi Mkuu wa Kenya yote nzima.

Na Sheikh wetu huyu aliifasiri hii Qurani kabla ya myaka 20 sasa; akachapisha juzuu kumi na tano na sura nyengine mbali mbali.

Alipoona haya yule mwanachuoni mkubwa wa Ki-Pakistani Sayyid Abul A'ala Mawdudy, aliazimia kulipokea yeye jambo hili na kuchapisha hii tafsiri ya Sheikh Abdulla Saleh Farsy.

Basi Islamic Foundation ikaitabiisha na kuitangaza kwa hima ya mwanachuoni mkubwa huyu Sayyid Abul a'ala Mawdudy.

Na Sheikh Abdulla Saleh akaipitia tena tafsiri yake yote nzima kabla ya kutabiishwa

chapa ya pili na akaongeza ya kuongeza na akasafisha ya kusafisha kwa mwisho wa jitihada yake ili iwe na nafuu kubwa na kusahihika kabisa. Lakini kinachofanywa na mwanaadamu hata kikitengenezwa vipi muhali kusalimika na makosa. Al-Kamaalu Lillahi Rabbil Alamyn.

Sasa Islamic Foundation inamshukuru Mwenyezi Mungu sana sana kwa kuwafikiwa kutekeleza muhimu mkubwa kabisa huu. Inastahiki Islamic Foundation ishukuru sana sana kwa kuwezeshwa na Mwenyezi Mungu haya kwani haya ndiyo yanayotakiwa kweli kweli kwa Waislamu kuyafanya.

Sasa namuomba Mwenyezi Mungu aitakabali kwao amali hii na aijaalie imekhalisika na iwe akiba yao ya kuwafaa duniani na Akhera.

Mpango wetu mwanzo kabisa ulikuwa hivi: (a) Tafsiri na Maelezo na Marejezo yawe ya Sheikh Abdulla Saleh Farsy; (b) Na kiwepo kitangulizi kirefu mwanzo wa kila sura kilichoandikwa na Sayyid Abul A'ala Mawdudy katika tafsiri yake kwa lugha ya Kiurdu inayoitwa *Tafhymul Quran.* Vifasiriwe vitangulizi hivyo kwa lugha ya Kiswahili; (c) Iweko katika mwanzo wa tafsiri dibaji ndefu, yake yeye Sayyid Mawdudy ya kufahamisha mambo muhimu yote yaliyohusiana na Qurani.

Katika mwaka wa 1969 wakati ilipochapishwa na kutangazwa chapa ya kwanza, Sayyid Abul A'ala Mawdudy alikuwa hajaimaliza tafsiri yake ya Kiurdu, nasi tuliona bora tusivitie vitangulizi vile alivyokuwa ashaviandika kama tulivyotaja katika (b); ili zisiwe baadhi ya sura zina vitangulizi na baadhi ya sura hazina. Mwaka jana, Sayyid Mawdudy kwa Rehema ya Mwenyezi Mungu aliweza kuimaliza tafsiri yake, lakini wakati huo tulikua tushaendelea sana katika kupitia upya chapa ya pili na kwa hivyo kufisafiri hivyo vitangulizi vya Sayyid Mawdudy kungetuakhirisha zaidi. Vile vile wasomaji wetu wamesubiri kwa muda mwingi sana, basi tulikata shauri kutoakhirisha zaidi utangulizi wa chapa ya pili. Sasa tuna furaha kwa kuwa kazi yenyewe imekamilika, lakini vile vile tunasikitika kwa sababu hatukuweza kuvitangaza hivyo vitangulizi vya mwanachuoni mkubwa huyo, Sayyid Abul A'ala Mawdudy. Inshaallah, vitatangazwa katika chapa ya nne.

Ama hiyo dibaji tuliyoitaja katika (c) tumeitia kwani ina faida isiyokuwa na kiyasi katika kufahamisha hakika ya Qurani na hakika ya ulingano wake na makusudio yake.

Katika chapa ya kwanza tuliwaomba wasomaji watuarifu makosa yoyote wanayoyaona katika tafsiri hii ya Qurani ili yasahihishwe katika chapa ya pili. Ijapokuwa tulipokea barua ya kwanza wiki mbili tu baada ya kuitangaza, siku nyingi zilipita kabla ya kuletewa maoni mbali mbali ya wasomaji tuliyoyataraji. Na kwa jumla wasomaji walipendezwa, lakini hatutawataja wale waliotusaidia kuisahihisha chapa ya pili maana wataweza wenyewe kuyaona masahihisho tuliyoyakubali. Tunawapa ahsanta kwa msaada huu wao.

Zaidi ya myaka miwili ilihitajika ili kuyapitia mashauri hayo ya wasomaji na mfasiri amewasubiri nasi tunataraji subira hii yake imevuta kheri. Kazi yenyewe ilikuwa kubwa sana wala haikutekelezwa isipokuwa kwa muawana wa Mwenyezi Mungu. La, sivyo, hatungeweza kuimaliza. Alhamdulillahi.

Kwa mara nyingine tafsiri ya Qurani imepatikana kwa lugha ya Kiswahili, safari hii katika nakala 25,000 ambazo tumesubutu kuzichapisha na Inshaallah tutatangaza na chapa ya nne katika siku zitakazo kuja, basi tunawaomba tena mutuarifu makosa yoyote muyaonayo au neno lolote ambalo tumeliacha.

Barua nyingi zimepokewa zenye ahsanta kwa sherehe iliyoandikwa na Sheikh Abdulla Saleh Farsy ili kuweka wazi itikadi ya Makadiyani na kuwatahadharisha jamii Islamu na khatari ya fitina iliyozuliwa na madhahabi hayo. Baadhi ya wasomaji wamesema kuwa Sheikh

Farsy amewashambulia watu hao pasi na kuwaonea imani yoyote. Ama wenye maoni haya tunawaomba watalii kwa makini mas-ala haya kabla ya kukata shauri. Baada ya kuyachunguza vilivyo, hawataweza kumwita Mirzai "Muislamu wa kweli" ilhali watu hawa wameukadhibisha mmoja katika misingi ya Uislamu. Yaani, wao wamejizulia "mtume mpya" aliyekuja baada ya Mtume Muhammad s.a.w. Je, watu hawa wamesoma Qurani na kuzingatia adhabu kali itakayowapata wenye kuligeuza neno la Mwenyezi Mungu kwa kufuata matakwa yao wenyewe?

Mahali kama hapa yafaa kutaja shauri lililokatwa mwezi 7, Septemba, 1974 na Serikali ya Pakistani, nchi wakaapo Makadiyani wenyewe. Baraza zote mbili zilipasisha Mabadilisho ya Katiba ya kukanusha Uislamu wa mtu yoyote yule asiyeamini kuwa Mtume wa Mwisho kabisa ni Muhammad s.a.w. au mwenye kudai utume baada ya Nabii Muhammad s.a.w. au mwenye kumuamini huyo adaiye kuwa ni mtume au mujadidi (mtengenezaji) wa dini. Kwa mujibu wa mabadilisho ya kifungu cha 106 cha Katiba, watu wa Kundi la Kadiyani na watu wa Kundi la Lahore wenye kujita "Waahmadii" sasa wametiwa katika orodha ya jamii zisizokuwa za Kiislamu.

Mambo haya yametokea mara tu kabla ya kupeleka chapa ya pili mtamboni na kwa hivyo Sheikh Abdulla Saleh Farsy alikuwa hawezi kubadilisha kwa namnaze sherehe yake kulingana na hali ya Makadiyani huko kwao, ambayo pasi na shaka utakuwa ni mwanzo wa kumalizika kwa madhahabi hayo ya upotevu. Dalili ya mvua ni mawingu!

Kazi ndefu ya kusoma muswada mara nyengine pamoja na kuchapisha tena na kutangaza tena haikuwezekana ila kwa msaada wa Mwenyezi Mungu. Tunamuomba awalipe wote waliotusaidia katika kazi hii ya kheri kama alivyowalipa waja Wake wengine wa kheri. Mwenyezi Mungu! Tutakabalie kama hao uliowatakabalia.

DR. MOHAMMAD SAYIED
Katibu Mkuu

THE ISLAMIC FOUNDATION,
P.O. BOX 30611,
NAIROBI, KENYA.
RAMADHAN 1394 (SEPTEMBA 1974)

DIBAJI

Mwanzo kushika kalamu — Naanza Kiislamu
Bismilla kukadimu — Na Alhamdu pamoja

Namsalia Bashiri — Na Alize At-hari
Na Sahaba wenye kheri — Na sisi sote pamoja

Namshukuru Rahimu — Neema zake adhimu
Kwa Jadidi na Qadimu — Nazishukuru pamoja

Na iliyopindukia mipaka — baada ya kunipa Uislamu — ni hii neema ya kuniwafikia kufasiri Qurani yote, kisha kuitabiisha, ipate kuwa kwangu Inshallah:—

(1) ILIMU YA KUDUMU NAFUU YAKE
Na iwe pia

(2) SADAKA YA MILELE
Na Inshaallah ataniwafikia vile vile

(3) KIZAZI CHEMA CHA KUNIOMBEA DUA

Muabudiwa kwa haki — Nitendee nitakayo
Nepukane na matayo — Iwe Kun Fayakunu

Kadiri nilitakalo — Nilipate kwa upesi
La kila hili na hilo — Yanijie kwa wepesi

Nakuombawe Quddusi — Ndiwe Muombwa Karima

Basi hii tafsiri ya Qurani iliyo SAHIHI: si ile iliyopotolewa Kusudi na kwa Inadi. Kwa hii, hiyo tafsiri potofu tunairudi. Na kabla ya hapa naliwazindua Waislamu wenzangu wa pande hizi — waliokaribia kupotolewa. Nikawatungia kitabu nilichokiita "Upotofu wa Tafsiri ya Makadiyani"[1] Na ilivyokuwa watu wa nchi zetu hizi hawamkubali mtu kuwa anaijua tafsiri ya Qurani ila awe kaipokea Tafsiri ya *Jalaleyn* kwa Mashekhe wenye kutegemewa, basi namshukuru Mwenyezi Mungu kusema kuwa mimi — Al Haqirulil Lahi taala — nina uhusiano kamili mashuhuri mtukufu na hao wenye kuipokea hiyo Jalaleyn; mmoja baada ya mmoja mpaka kwa hao wenyewe Kina Jalalud Din wote wawili:

(a) *Jalalud Din Al Mahally* — Aliyeifasiri tangu *Suratil Kahf* mpaka kumalizia sura ndogo ndogo, na ambaye alizaliwa mwaka 791 A.H. akafa mwaka 864 (kaishi miaka 73); na

(b) *Jalalud Din As Suyuty* — Aliyefasiri tangu *Al-Baqarah* mpaka mwisho wa *Subhana*, na ambaye alizaliwa mwaka 849 A.H. akafa mwaka 911 (kaishi miaka 62).

Sasa nautaja utungo wa hao mashekhe wakubwa mmoja baada ya mmoja mpaka kwa hao Mabwana Jalaleyn.

Nimeisoma tafsiri ya Sh. Al Mahally kwa:

(1) Sh. Al Amin bin Ali Al Mazrui
na yeye kwa (2) Sh. Suleiman bin Ali Al Mazrui
na yeye kwa (3) Sh. Ali bin Abdulla Al Mazrui
na yeye kwa (4) Sh. Abdulla bin Nafii Al Mazrui
na yeye kwa (5) Sh. Ahmad bin Muhammad Ad Dimyaty
na yeye kwa (6) Sh. Abdul Ghany Ad Dimyaty
na yeye kwa (7) Sh. Abdul Wahhab Al Bakhaty
na yeye kwa (8) Sh. Suleiman bin Umar Al Jamal
na yeye kwa (9) Sh. Muhammad bin Salim Al Hifny
na yeye kwa (10) Sh. Muhammad bin Muhammad Ad Dimyaty
na yeye kwa (11) Sh. Ali bin Ali Ash Shubramallisy
na yeye kwa (12) Sh. Ali bin Ibrahim Al Halaby
na yeye kwa (13) Sh. Ali bin Yahya Az Zayyaady
na yeye kwa (14) Sh. Muhammad bin Ahmad Ar Ramly
na yeye kwa (15) Sh. Zakariyya bin Muhammad Al Ansary
na yeye kwa (16) Mwenyewe Sheikh Jalalud Din Muhammad al Mahally.

Na nimesoma tafsiri ya Sheikh As Suyuty kwa:

(1) Sh. Ahmad bin Muhammad Mlomry
na yeye kwa (2) Sh. Ali bin Abdulla Al Mazrui
na yeye kwa (3) Sh. Abdulla bin Nafii Al Mazrui
na yeye kwa (4) Sh. Ahmad bin Muhammad Ad Dimyaty
na yeye kwa (5) Sh. Abdul Ghany Ad Dimyaty
na yeye kwa (6) Sh. Abdul Wahhab Al Bakhaty
na yeye kwa (7) Sh. Suleiman bin Umar Al Jamal
na yeye kwa (8) Sh. Muhammad bin Salim Al Hifny
na yeye kwa (9) Sh. Muhammad bin Muhammad Ad Dimyaty
na yeye kwa (10) Sh. Ali bin Ali Ash Shubramallisy
na yeye kwa (11) Sh. Ali bin Ibrahim Al Halaby
na yeye kwa (12) Sh. Ali bin Muhammad Al Ujhury
na yeye kwa (13) Sh. Burhan bin Abdul Rahman Al Alqamy
na yeye kwa (14) Sh. Muhammad bin Abdul Rahman Al Alqamy
na yeye kwa (15) Mwenyewe Sheikh Jalalud Din Abdul Rahman As Suyuty.

Na nimezisoma vyema vile vile Tafsiri zote mbili hizi kwa:

Sh. Abubakr bin Abdulla Bakathir na kwa Sh. Muhsin bin Ali Al Barwany na wao
kwa (2) Sh. Abdulla bin Muhammad Bakathir
na yeye kwa (3) Sh. Umar bin Abi Bakr Bajunaid
na yeye kwa (4) Sayyid Ahmed bin Zeiny Dahlan.

Na yeye kwa mtu mmoja mmoja vile vile mpaka kwa hao Kina Jalaleyn wote wawili. Nilisema-na ninasema-'Nina uhusiano kamili mashuhuri mtukufu na hao wenye kuipokea

hiyo Jalaleyn', lakini sikusema kuwa nitaifuata tafsiri ya kina Jalaleyn neno kwa neno. Wao ni wanadamu kama wanadamu wengine; wana mahali walimokosea katika hii tafsiri yao na vitabu vyao vyengine, khasa Jalalud Din Suyuty; kama yalivyobainishwa haya katika vitabu vingi khasa katika Sahifa 124 ya An Nuris Safir na katika kitabu chote cha Al Mughyr.

Na mimi — *Al Hamdulillah* — nimeisomesha hii Tafsiri ya Jalaleyn kwa darasa kubwa za Msikiti Baraza tangu mwaka 1363 (1944). Na mpaka nilipoondoka Unguja Julai 1967 ndiyo darasa yangu ya maisha mwezi wa Ramadhani hapo Msikiti Baraza na kila Al Khamis na Ijumaa, pamoja na Hadithi za Mtume na Tarikhi ya Mtume na za watu wakubwa wa dini na yaliyo kama haya.

Na hamu yangu kubwa ilikuwa nisife kabla sikuifasiri Qurani yote na kuitabiisha. *Al Hamdu Lillahi Rabbil Aalamyn.*

Tutimizie yatimu — Tunayoyakusudia
Ya Wasial Ataya — Dua tutakabaliya

Wallahi Billahi — Sikuyawaza
Na moyoni mwangu — Sikwelekeza
Haya ni ya Mola — Yake majaza
Aliyonijazi — Mola Manani.

Nawashukuru na ndugu zangu maazizi wa The Islamic Foundation walioitabiisha na wasaidizi wao. Na mkubwa wao ni Allamatul Kabir Mawlana Sayyid Abul A'ala Mawdudy. Mwenyezi Mungu awape kila kheri za dunia na Akhera. Wao ndio sababu hata yakapatikana haya ya kutoka leo hii tafsiri kamili Sahihi ya Qurani.

Tafsiri njema — Hii inatoka
Isiyo kilema — Na kutetereka
Kwa yako Neema — Mola Msifika
Rabbi tuongeze jaha — Utuzidishe furaha
Utondolee karaha — Ya wenye kutufanyia
Tena uzidi umuri — Na kila mambo ya kheri
Utuepushe na shari — Kwa enzi yako Aliya
Tuhifadhi waja wako — Na viroja na vituko
Ili tukae kitako — Kwa nyoyo kututulia
Na Akhera tutukuke — Peponi kwako tufike
Palo pema utuweke — Pamoja na Manabiya
Rabbi takabali duwa — Mikono tunainuwa
Tuongezee uluwa — Na afuwa na afiya
Alhamdu Lillahi — Mola asiye shabihi
Jioni na asubuhi — Namhimidi Jaliya

Na mimi nimeanza kutabiisha tafsiri ya Qurani kabla ya hao Makadiyani. Nalitabiisha katika Mfungo Sita mwaka 1369 (Januari, 1950) "Sura za Sala na Tafsiri Zake". Nikatabiisha katika Mfungo Nne, 1370 (Octoba, 1950) "Tafsiri ya Baadhi ya Sura za Qurani — *Yasin, Waqiah, Mulk.*" Nikatabiisha "Tafsiri ya *Suratul Kahf*". Kisha nikaanzisha mpango wa kutoa tafsiri ya Juzuu moja moja tangu tafsiri ya *Suratul Baqarah* mpaka nilipofika. Na mwanzo wa kutoka tafsiri ya Makadiyani ni 11.3.53 kama ilivyo katika tafsiri yao. Sasa walioiga ni sisi au ni wao? Tungekuwa sisi sio wenyewe tungeyajuaye tukayafanya? Na mwenye macho anaona mwenyewe, hata akijigambaje huyo Mjigamba. *Alhamdu Lillah.*

Na katika tafsiri yetu hii — kama atavyoona kila mtu *Inshaallah* — iko (a) Tafsiri na (b) Maelezo chini yake kwa Aya zinazohitajia maelezo. Na sana kabisa tumeshughulikia mambo yaliyohusiana na Tawhidi ya Mwenyezi Mungu kwani Uislamu wote uko hapo. Hilo ndilo shina. Likioza utaoza mti wote, uanguke. Na pia tunatia "Marejezo ya Upotofu wa Tafsiri ya Makadiyani".

Na mwanzo kabisa Inshaallah utaona Dibaji kubwa kabisa iliyokusanya kila anayoyahitajia mtu kuyajua katika Qurani — ambayo labda yakimsumbua. Ataona, vizuri kabisa yamepembuliwa. Aseme:

"Alaa! Haya ambayo ilikuwa katika moyo wangu niyajue, nimetajiwa na vizuri nimebainishiwa."

Na Dibaji hiyo — *Msingi wa Kufahamu Qurani* — ni ya Mawlanal Mawdudy.

Na katika ambao lazima niwashukuru, dhahir shahir, ni ndugu yangu — mzizi wa roho yangu, mpiga kelele za dini mwenzangu aliyekuwa, Kadhi Mkuu wa Kenya kabla yangu, Sheikh Muhammad bin Kasim Mazrui. Mwenyezi Mungu ampe nguvu aendelee na aliyonayo.

Na maelezo ya Juzuu ya *Amma* — isipokuwa Marejezo ya Makadiyani — yake yeye na ndugu yake, Marehemu Sh. Rashid Kasim.

Nataka ile tu — Daraja yangu
Sitaki nyingine — Kama wenzangu
Sinui mikono — Kashika mbingu
Amenipa mengi — Mola Karima.

Kwa vile mwanaadamu si mwenye kukamiiika, basi nimeipitia tena tafsiri yangu na kuyasahihisha yenye makosa ili chapa hii ya tatu izidi kuwa sahihi. Baada ya kutoka chapa ya kwanza nilifurahi sana kupokea barua za wasomaji pamoja na mashauri yao wala sikuacha kuyazingatia. Lakini hii chapa ya tatu vile vile — juu ya jitihada yote iliyopitishwa — haitakosa makosa. Kila kisichofanywa na Mwenyezi Mungu lazima kiwe na makosa japo kidogo japo jitihada gani ikipita kama alivyotwambia Mwenyezi Mungu katika Aya ya 82 ya *Suratin Nisaa* (Sura ya 4). Basi ninawanasihi wasomaji wa chapa ya tatu waniletee maoni yao ili yazingatiwe wakati wa kuitangaza chapa ya nne, Inshallah.

ABDULLA SALEH FARSY,
Kadhi Mkuu wa Kenya.

P.O. Box 81760,
MOMBASA, KENYA.
MFUNGO TISIA, 1394 (July, 1974).

PONGEZI

Naanza kumuhimidi *Mola Rahimu Wadudi*
Mwenye sifa Mahmudi *Asiyekuwa na Tama*
Tena ninamsalia *Mtume wake Nabiya*
Na Ali zake pamoya *Na Sahabaze Kirama*
Kisha niwageukie *Ndugu zangu niwambie*
Hela tukizingatie *Chuo cha Mola Karima*
Kimeletwa kutufunza *Na ndia kutuongoza*
Na ungi wa maliwaza *Twafahamu tukisoma*
Amebaini Qahari *Ndia za kheri na shari*
Kuwaongoza Bashari *Na kuwaokowa Umma*
Tungekuwa Ashirafu *Na Mabwana watukufu*
Unyonge na udhaifu *Usingelituegema*
Ila kwa kutofahamu *Maneno yake Karimu*
Ummati wa Isilamu *Umesiri kuwa nyuma*
Alipowaona Waja *Wana dharura na haja*
Kijana cha Kiunguja *Alisimama kwa hima*
Kufasiri Quruani *Na kubaini Ma-ani*
Kwa lugha yetu ya Pwani *Sinina na A-awama*
Akafungua Kunuzi *Za hakika na majazi*
Yote kayaweka wazi *Hapana asichosema*
Mepambanua Shiriki *Upotofu na Nifaki*
Na Dini safi ya haki *Kwa mwenye kuiandama*
Wanajeshi wa shetani *Watakuwa mashakani*
Wamshitakie nani *Wote wamehalimama*
Wazi wazi mebaini *Uzuzi wa Kadiani*
Haina tena thamani *Fasiri yao dhamima*
Kuisikia harufu *Mirizai wapotofu*
Wameingiwa ni khofu *Nyoyo zimewaangama*
Na sasa nitasarihi *Jina lake Muslihi*
Ni Abdullahi Salihi *Farisi wa zetu zama*
Fununi amezihozi *Za Kitabu Li-azizi*
Na nyengine kama hizi *Za Nathiri na Nudhuma*
Huku kwetu Sawahili *Hakuna Sanadi Ali*
Kufikia kwa Jalali *Kuliko yake Allama*
Ya Rabbi umbakishe *Umri mtawilishe*
Sote utunufaishe *Kwa yake Ilimu njema*
Mahasidi mkifie *Shari yao mwepushie*
Wavunde wasibakie *Amina Mola Karima.*

MUHAMMAD KASSIM MAZRUI,
(Kadhi Mkuu Wa Zamani)

MSINGI WA KUFAHAMU QURANI

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu aliyesema katika Qurani yake kuwa "Imekujieni — kutokana kwa Mwenyezi Mungu — nuru (kubwa) na kitabu (kitukufu) kinachobainisha (kila linalohitajiwa)". Na Rehema Zake na Amani Zake zimwendee Mtume wake, Bwana Muhammad, Mwisho wa Mitume wote, na ziwaendee Jamaa zake na Sahaba zake wote.

Vitabu vyote tunavyosoma tunaona ndani yake kuwa kila yanayotajwa humo — katika maelezo na fikira na hoja — yanakhusika kwa jambo makhsusi, na kwa mpango wa utungaji makhsusi na kwa kuendeleza hayo anayoyataka huyo mtungaji.

Basi kwa ajili ya kuzoea haya yule mtu anayeanza kuvisoma, akaona kuwa kitakuwa kama hivyo — yamekwisha kupangwa mbali mbali makusudio yake, na yametengwa katika milango mbali mbali, ili aisome kila habari mahala pake. Na anadhani kuwa ataona kila jambo katika mambo yanayokhusiana na uhai wa binaadamu limepangwa peke yake kwa mfuatano wake.

Lakini akianza kusoma Qurani kwa kuzingatia ataona kinyume cha alivyodhani. Ataona mambo yaliyokhusiana na *Itiqadi* na mambo yaliyokhusiana na *Akhlaqi* (tabia nzuri) na mambo yaliyokhusiana na Sharia na ya Ulingani wa dini na ya Nasaha na ya Mazingatiyo na ya Kutoa makosa na ya Kulaumu na ya Kukhofisha na ya Kupendezesha na ya Hoja na Dalili na ya Visa vya mambo yaliyopita na ya Ishara zinazopatikana kwa kutazama alivyoumba Mwenyezi Mungu kwenye mbingu na ardhi; ataviona vyote hivi kunakaririka kubainishwa kwake mara kwa mara, na huanzwa — na hurejezwa — utajo wake kwa namna mbali mbali.

Utaona Qurani inataja kitu, mara — hiyo — imezukia kitu kingine na chengine na chengine; na wakati mwingine kwa mzukio wa ghafla. Basi hutokea ikawacha dhamiri ya msemezwa ikatumia dhamiri ya kitu kinachotajwa habari yake au dhamiri nyinginezo au mpango mwingineo.

Ama kugawiwa Qurani katika mambo makhsusi na milango makhsusi, hili halimo kabisa.

Yakitajwa mambo ya tarikhi hayatajwi kama yanavyotajwa katika vitabu vya Tarikhi. Na yakitajwa mambo ya *Philosophy* au *Logic* au *Nature Study* na mengineyo, hayatajwi kwa lafdhi zinazotumiwa humo. Na yakitajwa mambo yaliyokhusika na Mambo ya Wanaadamu au ya Siasa na Iqtisadi na ya Kanuni na Hukumu, haitaji kwa lafdhi hizo. Na ikitaja habari ya Akhlaqi na mwendo mzuri, hutumia mpango ambao sio uliozoewa kutumiwa.

Basi msomaji Qurani ili aijue ndani yake, akiona hivi — ambavyo sivyo alivyozoea kuona katika vitabu vingine — hushituka akaona kuwu kitabu hiki kimekosa mpango mzuri, na maelezo yake yamebaraganyika ovyo katika vifungu visivyokuwa na mfuatano.

Basi anayeisoma hii Qurani, na hali ya kuwa hataki kuiamini, ila anataka kupinga tu na kuleta matatizo, anapata fursa nzuri ya kutolea pumzi zake hizo. Lakini anayeisoma na hali ya kuwa anaiamini na anainyenyekea, humvuta kabisa hiyo migeuko yake ya mara kwa mara. Mara akawacha matakwa haya, mara ukatulia moyo wake kwa hayo, mara akapata natija nyingine nzuri nzuri kwa yale; hata huwa kama kila Aya imejitenga na mwenziwe kwa namna ya peke yake wenyewe, nzuri kabisa kama ile ya mwenziwe. Mambo mapya mapya yanamzukia.

Akitaka mtu kukijua kitabu cho chote kile kilivyo, lazima kwanza ajue nini makusudio ya kitabu hicho na nini khasa matakwa yake makhsusi katika kitabu hicho, na ajue vile vile mbinu za mwandiko wake na namna ya lugha yake inavyotumiwa, na ajue undani wake khasa

ni nini. Na vitabu vingi tunavyovisoma hatupati tabu katika kutambua haya.

Lakini katika Qurani hatuwezi kuyapata haya kwa upesi tuliouzoea. Kwa hivyo mtu akisoma hii Qurani kama anavyovisoma vitabu vyingine hawezi kupata khasa makusudio yake na upeo wa jambo lake khasa; na anaustaajabia mpango wake na usimuliaje wake, na hajui kwa nini ikawa hivyo — juu ya kuwa anapata hikima tukufu kabisa zilizomo katika hii Qurani; lakini hapati undani wake khasa, ingawa anapata anayoyapata.

Bali kuna watu wengine wametatizika kwa kusoma hii Qurani bila ya ujuzi wa kawaida zake za kuifahamia, wakababaika kwa ile mimeremeto yake inavyomeremeta huku, ikameremeta kule, pası na kutambua wao sababu za kuteremka Aya hizo; basi wakababaika.

Inataka kwanza mtu ajue hii Qurani mpango wake ni vipi kwa mkabala wa vitabu vyingine, Na vipi imeteremka, Na kwa nini ikaja kwa mpango huu, Na inasema juu ya habari gani, Na yepi khasa mambo yake muhimu. Akiyajua mtu haya kwanza atasalimika na kuteleza njiani au kujikwaa; na zitamfunukia njia nyingine za kuifahamu.

Basi anayetaka kuisoma Qurani aione imefuata mpango wa vitabu vyingine — akawa anahangaika humo aone hivyo, wala hataona — huyo hakuujua msingi wa Qurani na kawaida zake. Anaona kuwa hiyo Qurani ni Kitabu cha Dini tu basi; na anakisawiri kitabu hiki kama vitabu vyingine na anaisawiri dini hii kama dini nyingine; kama wanavyofanya watu wengine.

Basi anapoona haya asiyodhani, haoni raha na huwa anahangaika kupekuapekua ndani ya Msahafu mzima, labda ataona hayo aliyoyadhani; kama mgeni anayehangaika katika njia za mji alioushukia asioujua.

Na angesalimika na haya lau angejuwa mbele kuwa kitabu hiki ni cha namna yake peke yake katika utungo wake, hakina mwenziwe katika mpango wake wala katika kule kuchaguwa mambo kwake. Basi huo muandiko unaoudhani wewe, ulioutia kichwani mwako kwa kuona vitabu vyingine, haukusaidii kufahamu kitabu hiki hata chembe, bali unakuzuilia kukifahamu.

Basi ukitaka kuifahamu Qurani, baidisha katika fikira yako kila uliyoyathubutisha humo uliyoyazoea katika vitabu vyingine, uelewe vizuri na mipango mipya na mizuri iliyo katika kitabu hiki.

Inampasa kila mwenye kutaka kujifunza kitabu hiki ajue — kabla ya cho chote kile — msingi wa Qurani; ikiwa anaiamini au haiamini. Maadam anataka kukifahamu basi lazima ayajue hayo ili apate kuondokea hapo. Ajue msingi wake alioubainisha Mwenyezi Mungu na alioubainisha Mtume wake. Nao ni huu.

(1) Mwenyezi Mungu Mwumba wa Ulimwengu wote huu — akautawala akawa anauhukumu anavyotaka — amemuumba binaadamu akamweka katika hii sehemu inayoitwa Ardhi ambayo ni sehemu ndogo mno kabisa katika sehemu chungu mno kabisa za Mamlaka yake yasiyokuwa na upeo wala mpaka. Na amempa huyo binaadamu uweza wa kupatia ilimu na akampa fikira na kufahamu na akamuezesha kutambua jema na baya na akampa huriya ya kutaka au kukataa (kufanya na kuacha) na kusarifu mambo yake kama anavyotaka, na akampa istiqlali kidogo ya kupitisha hata yasiyokuwa yake na akamfanya ndiye mfalme wa ardhi.

(2) Na akamtia ilhamu ya nguvu kabisa katika moyo wake kuwa Mungu anamwambia Mimi (Mungu) ndiye Mola wako na Mola wa ulimwengu wote, na Mimi ndiye Mungu wako na Mungu wa ulimwengu wote, na Mimi ndiye Mfalme wako na Mfalme wa ulimwengu wote. Usiwe katika ulimwengu wangu huu huru kabisa kabisa, umetakabari unafanya unavyotaka wala hujali. Wala usiwe mtumwa wa asiyekuwa miye; hakuna asiyekuwa miye anayestahiki kumuabudu, kumtii na kumnyenyekea. Na huu uhai uliopewa ndani yake Huriya kidogo,

ndio wakati wa mtihani; utarejea kwangu baada yake, nitazame uliyoyafanya; niwapambanue wepi waliofuzu na wepi walioanguka. Na njia nzuri ya kufuata ni hii:

"Nifanye Mimi ndiye Mola wako peke yangu na ndiye wa kukuhukumu peke yangu. Ufanye amali zako kama nilivyokuongoza; na uishi hapa duniani, na hali ya kuwa unajua kuwa umo ndani ya mtihani, na jitihadi yako yote upasi. Na ukenda kinyume na haya basi kila mwendo unaouenda ni wa makosa tu. Na ukifuata ule mwendo wa kwanza — na wewe ni Huru katika kuufuata mwendo huo, hakuna cha kukuzuilia — si utastarehe hapa tu duniani na kutua moyo wako, bali Nitakupa neema kubwa kabisa utakaporejea kwangu katika hapo mahala panapoitwa Pepo. Upate neema ya daima na raha ya milele bila kuchoka wala kutaabika. Na ukifuata huo mwendo mwingine — na wewe ni Huru katika kufuata mwendo huo pia — basi si utapata balaa na shari na kuangamia papa hapa duniani tu, bali Akhera utakwenda Motoni uipate adhabu ya milele na machungu ya daima na ghamu isiyokwisha."

(3) Mwenyezi Mungu amewaweka binaadamu hapa katika ardhi baada ya kuwatengezea yale tuliyoyataja. Akawaleta wale watu wawili wa mwanzo — Adamu na Hawa. Na akawaongoa kwa uwongozi wake ili waufuate wao na kizazi chao mpaka mwisho wa ulimwengu. Hakumwumba mtu katika kiza na ujahili. Bali kamleta ulimwenguni kwa nuru na ilimu. Akawa huyo mtu wa mwanzo anajua nini haki, na akafundishwa yanayohitajiwa katika uhai huu. Nayo ni taa (kutii) ya Mwenyezi Mungu (Uislamu).

Na yeye akawausia wanawe na kizazi chake chote kuwa wasimwabudu ila Mwenyezi Mungu na wasife ila katika Uislamu. Lakini baada ya miaka mingi aliingia kuiacha njia hii ya haki na kufuata njia zilizo potoka na kwenda upogo. Na wakapotea na kumjua Mwenyezi Mungu vilivyo, ima kwa kutomjali au kwa kumkanusha, wakamfanyia Mwenyezi Mungu chungu ya washirika katika viumbe vya ardhi na mbinguni; wengine wa kuonekana na wengine wamo katika fikira zao tu; na wengine wa kibinadamu na wengine viumbe wengine. Na ile ilimu ya haki waliichanganyishia namna namna ya mambo yaliyokhusu *Philosophy* na ilimu nyingine zisizokuwa za kutegemewa. Basi yakazuka chungu ya madhehebu yasiyokuwa na idadi na wakaitupa nyuma ya migongo yao haki waliyopewa — Sharia nzuri, Akhlaqi nzuri, Ustaarabu na mengine ya kutengeneza dini yao na itengenee Akhera yao pia. Wakafanya — kwa matamanio yao na asabia yao (kuvutia maslaha ya jamaa zao) — njia nyingine za kujiendesha ambazo zilijaza ardhi dhulma na fisadi na kuharibikiwa na kuangamia.

(4) Na ile Huriya ya kiasi maalumu aliyopewa mwanadamu haimpelekei Mwenyezi Mungu kumrejeza — kwa nguvu — aliyepotea ili ende njia sahihi, akitaka asitake. Na ule muda aliompa wa kuishi haumpelekei Mwenyezi Mungu kwenda kumwangamiza mara moja kwa kuwa anakhalifu amri zake. Kisha Mwenyezi Mungu akajiwajibishia — tangu mwanzo wa kuja Ubinaadamu — kuwatengenezea wanaadamu njia ya kuwaongoza katika huu uhai wao. Na akawachagua Mwenyezi Mungu kwa Irada yake watu katika wanaadamu; wememuamini vilivyo wakafuata anayoyapenda, akawafanya wajumbe wake. Akawapelekea Ujumbe wake na akawaletea ilimu ya haki; akawafundisha njia njema ya kuongoza. Tena akawaamrisha wawalinganie wanaadamu wenzao kufuata njia iliyonyoka waliyoitupa na kuiwacha.

(5) Mitume hawa wakapelekwa kwa watu mbali mbali na nchi mbali mbali. Mwenyezi Mungu akadumu kuwaleta tu tangu alfu ya miaka baada ya miaka, hata idadi yao ikawa alfu nyingi. Na wote walikuwa juu ya dini moja — mwendo ule ule aliokuja nao yule binaadamu wa mwanzo alipoteremka kwenye ardhi. Wakawa wanaufuata uongozi ule ule katika Sharia na Akhlaqi na Ustaarabu. Na makusudio yao yalikuwa mamoja. Nayo ni kuwaongoza

wanaadamu katika dini ya Mwenyezi Mungu na uongozi Wake. Basi wale waliokubali mwendo wao walichanganyika wakawa uma mmoja unaofuata hukumu za Mola wake na kutii njia yake. Na wakajipania kuwazuilia wengine kukhalifu mwendo huo mzuri. Basi hao Mitume walijipania barabara kufikisha kweli kweli Ujumbe waliopewa. Lakini wengi wa watu hawakuwafuata. Na waliowafuata waliingia kidogo kidogo katika kufisidi na kupotea. Kuna wengine waliopotea kabisa kabisa. Na kuna wengine walioyágeuza maneno ya Mwenyezi Mungu wakayaandika kwa namna waipendayo wao.

(6) Na mwisho kabisa (katika uma wa mwisho) akaletwa Nabii Muhammad katika ardhi ya Waarabu kwa ile ile kazi waliyoletwa Mitume wengine waliotangulia. Kukawa kulingania kwake ni kulingania wanaadamu wote pia hata wale waliokuwa wafuasi wa Mitume waliotangulia wakapotea njia. Ikawa kazi yake ni kuwalingania wanaadamu wote wende njia iliyonyoka ya uongozi wa Mwenyezi Mungu. Wakawa wale walioamini ulingano huu ni Uma Mmoja unaofuata ulingano wake; na wakawalingania wengine kufuata ulingano huo wa kuwatengenezea dunia yao, ili itengenee na Akhera yao pia.

Na hii Qurani ndicho kitabu cha kulingania hayo na Uteremsho wake Mwenyezi Mungu juu ya Nabii Muhammad, uwe uwongofu na nuru ya kuongozwa anaowataka katika waja Wake.

Basi baada ya kwisha kujua msingi wa Qurani, kutakuwa kwepesi kwake kufahamu hakika ya kitabu hiki na lipi la kulitafuta ndani yake.

Mapendeleo ya Qurani

Kumwongoza mwanaadamu — kumbainishia lipi la kumpa kufuzu na raha na lipi la kumletea khasara na tabu.

Mabainisho yake

Kubainisha kuwa hizi Sharia walizozizua wanaadamu — za kumkhusu yeye mwenyewe na uhai wa duniani na mpango wa ulimwengu na Dhati ya Mungu — wamezizua kwa ilimu yao ya juu juu na kukadiri tu kwao na kufuata matamanio ya nafsi zao. Basi yote hayo ni batili kwa hakika, na yenye kumwangamiza mwenyewe mwanaadamu mwisho wake. Ya haki ni yale ambayo Mwenyewe Mwenyezi Mungu amemfundisha mwanadamu alipomleta ulimwenguni akamfanya wa kukaa hapa. Basi kwa mujibu wa hayo hapana njia iliyonyoka zaidi na inayoleta mwisho mwema kuliko hiyo njia iliyonyoka aliyoifundisha Mwenyewe Mwenyezi Mungu.

Lengo la Qurani

Kumlingania mwanaadamu kuifuata njia hiyo Sahihi na kumbainishia uwongozi wa Mwenyezi Mungu aliouacha kwa kutojali kwake au aliouharibu kwa kujiona kwake na kughurika kwake.

Anayeisoma Qurani — akayaweka haya matatu mbele ya macho yake — itambainikia bila ya kificho kuwa hii Qurani haikuacha Mapendeleo yake wala Mabainisho yake wala Lengo lake hata chembe. Na ataona matajo yake ya kila namna yanakamatana na yale mabainisho yake, kama zinavyokamatana katika kidani lulu zake kubwa na lulu zake ndogo. Mara utaiona inasema habari za mbingu namna zilivyofanywa, na binaadamu namna alivyoumbwa, na mazingatio yaliyomo katika hii ardhi na uma zilizopita na visa vyao. Na mara utaiona inakosowa vitendo vya uma mbali mbali na nyendo zao na itikadi zao. Inabainisha mambo yanayoonekana na mambo yasiyoonekana. Siyo kumfundisha binaadamu

Nature Study wala *History* wala *Literature* wala yaliyo kama haya. Bali imekuja kumwondoshea kuikosa ile njia Sahihi aliyoongozwa, na kumthibitishia uhakika wake, na kuwafahamisha natija nzuri inayopatikana katika kufuata hiyo njia Sahihi, na natijia mbaya inayopatikana katika kuikhalifu hiyo njia ya haki. Kwa hivi haisimulii — haya ya *Nature Study* na tuliyotaja baada yake — po pote pale ila kwa namna inayonasibu Lengo lake. Na dasturi yake hii Qurani, haitaji mambo hayo ila kwa kadiri ya haja tu, kisha hurejea katika Lengo lake lile lile. Basi masimulizi yake yote yamo katika Tablighi — kulingania Dini Sahihi na mwendo mzuri.

Na vigumu kuufahamu mwendo wa Qurani na mpango wake maadam hujui kuteremka kwake.

Qurani si kitabu alichoteremshiwa Nabii Muhammad kwa mara moja kwa pamoja, akaambiwa awatangazie watu na awalinganie kufuata yaliyomo ndani yake ya kuendesha maisha yao, Wala si kitabu kilichofikiriwa kikapangwa kwa mpango wa vitabu vya dasturi. Kwa hivi huoni ndani yake ule mpango wa dasturi ya vitabu. Kitabu hiki namna yake peke yake.

Mwenyezi Mungu amemchangua Mtume wake huyu katika mji wa Makka — mmoja katika miji ya Baraarabu — atangaze Ujumbe wake. Akamwamrisha awaanze kwanza jamaa zake na kabila yake walio katika mji wake. Nao ni Maqureshi. Akamfundisha yepi ya mwanzo kuyafanya katika jambo hili. Na makubwa katika hayo ni haya matatu:—

(1) Kumfundisha yeye mwenyewe Mtume kujiweka tayari kwa jambo hili na awe wa namna gani.

(2) Kujua yale ya mwanzo kabisa katika hii haki, na hakika ya mambo, na kuyavunja hayo waliyokuwa nayo hao waliokuwa pamoja naye, katika kuikosea haki ya duniani na Akhera.

(3) Kuwalingania kwenda hiyo njia Sahihi na kubainisha akhlaqi zake zilizokamatana na uwongozi wa Mwenyezi Mungu ambazo zikifuatwa ndio itapatikana raha na kufuzu.

Ule Ujumbe wa mwanzo, maneno yake yalikuwa yamekusanya mambo mbali mbali yanayotajwa kwa ufupi, yanayowafikiana na ule wakati wa mwanzo. Lugha nzuri kabisa, yenye maana matukufu kabisa, yenye ladha kubwa mno kabisa na taathira ya kuthubutu kabisa; kwa msimulio unaowafiki dhauqu zao; ili yagande barabara katika nyoyo zao na yathubuuti vyema katika vifua vyao, na yaone raha kabisa masikio kuyasikia, kwa ule mpendezo wake, na iwe lazima ndimi kuyasoma, kwa ile ladha ya kutamka alfadhi zake, kwa mpango wake ule wa ajabu. Na mambo hayo yanayotajwa yakiwafiki hali zao za mahala pao hapo, ingawa yanawaenea watu wote wa ulimwengu mzima daima milele; lakini hizo dalili zake na stishhadi zake zikitolewa kwa yanayopita hapo. Linatiwa na linaondolewa hili na hilo na lile na jinginelo, likatajwa kwa taathira kubwa mno kabisa. Mambo ya Tarikhi yaliyomo humo ni ya Tarikhi yao. Na mazushi yaliyotajwa humo ni mazushi yao na ada zao. Na mazingatio yanayotajwa humo ni athari na mazingatio ya wanayoyaona kwa macho yao. Na makatazo yanayokatazwa ni makatazo ya Itikadi zao mbaya na Tabia zao mbovu na Aibu zao chafu. Yametajwa hivi ili yaathiri katika nyoyo zao na mabongo yao.

Umeendelea mpango namna huu kiasi cha miaka mine mitano. Na taathira iliyopatikana katika muda huu inadhihiri katika mambo matatu haya:—

(1) Waliuamini ulingano huu baadhi ya watu watukufu wa hapo, wakawa ndio chanzo kizuri cha uma huu wa Kiislamu.

(2) Ikasimama sehemu kubwa kabisa ya watu kuupinga ulingano huu, ima kwa ujinga

wao au kwa hawa (mapenzi) ya nafsi zao tu na maslaha yao, au kwa kule kuking'ang'ania kwao kila walichowakuta nacho wazee wao.

(3) Ukaingia Ulingano kutoka nje ya Makka.

Basi hapa unaanza Ulingano huu daraja yake ya pili. Ukawa msongamano mkubwa kabisa baina ya Uislamu na huo ukafiri wao waliourithi kwa wazee wao. Ukadumu muda wa miaka minane au tisaa Wala si Makka tu wala kwa Maqureshi tu basi, bali kila aliyetaka ukafiri wao uendelee mbele alipania kuupinga Ulingano huu. Bara Arabu nzima ikauumia meno barabara kwa mwisho wa uweza wake. Wakatumia kila njia na kila kitimbi kuuvunja ulingano huu. Wakawa wanatumia Propaganda ya kusema uwongo, Kuusingizia usiyoyasema, Kuupinga bure bure, Kuwatilia watu shaka, Kuwazuilia wageni wasimsikilize Mtume wala kukutana naye Wakawavamia wale waliosilimu kwa namna za dhulma na adhabu na ukatili. Wakawakata kabisa na wakawadhikisha mno, hata ikawapasa wengi katika hao wahame hapo, wawache nchi yao na mali zao kwenda nchi ya Mahabushia mara mbili. Na mara ya tatu wakahamia Madina. Na juu ya taabu kubwa hizi na kupingwa kukubwa huku, ulingano wa Uislamu ulikuwa unaendelea tu, na ikawa hapana nyumba moja katika nyumba za Makka ila yuko aliyesilimu. Na lililozidi kuwatia uchungu na kuwapandisha mori ni kumuona katika wao: ndugu yake mwenyewe au mwanawe mwenyewe au mjukuu wake mwenyewe au mkewe mwenyewe au shemeji yake mwenyewe au . . . ameingia katika Uislamu na anaufia uchungu kweli kweli na anaufidia kwa roho yake na mali yake na kila chake kilicho thamini. Wakaona watoto wao wenyewe waliowatoa migongoni mwao wanawapinga kwa dhati yao. Na katika ajabu ni kuwa hawa iliowapasa wawakate sasa, wawe hawana shughuli nao, ndio wale ambao kabla ya hapo wakiwaona ndio nguzo zao na pambo la mkusanyiko wao. Na wakawa sasa wanaoingia katika huu ulingano wa Uislamu wanafikilia katika kutengenea na ukweli na tabia nzuri daraja ambayo iliwashangaza walimwengu wote, hata wakayakinisha kuwa Ulingano huu ni ulingano wa kweli na unatoa WATU wa KWELI.

Na katika muda huu wa ushinde mkubwa kabisa huu, Mwenyezi Mungu alikuwa akiteremsha — kwa minasaba mbali mbali — khutuba (Aya) kali na zenye taathira kubwa kama mito yenye nguvu na mifuriko mikubwa na nyoto kali kabisa. Katika Aya hizi wakafundishwa Waislamu wajibati zao za mwanzo, wakatiwa Hamasa barabara, na wakafundishwa Ucha Mungu wa kweli na tabia tukufu na usafi wa kweli, na wakaonyeshwa namna ya kuitangaza hii dini iliyonyoka sawa sawa, na wakashajiishwa walinganie; kwa waadi wa kweli wa kufuzu kwa kuipata Pepo yenye neema za daima. Wakahimizwa waipiganie kwa subira kubwa na kusimama barabara kwa nyoyo thabiti. Wakajazwa shauku ya kujitolea na kutoa kila cha rahisi na ghali, bali na roho pia; kwa kuupeleka mbele ulingano huu. Wakajazwa Hamasa hiyo hata wasijali shida yo yote ile, hata ikiwa kubwa vipi. Na walionywa barabara wale waliokufuru na kung'ang'ania yale waliyokuwa nayo, wakampiga vita Mtume na ulingano wake huu, wakaikataa haki na wasizingatie yaliyowapitia watu na uma zilizopita, na walikuwa wakijua habari zao, wakipita mchana na usiku katika safari zao katika miji hiyo yao. Na wakaonyeshwa dalili za Akhera kwa mambo wanayoyaona kwa macho yao; katika mbingu na ardhi, na wakayahisi khasa katika nafsi zao na maisha yao ya kila saa na wakati. Wakabainishiwa ubatilifu wa ushirikina wao na kukataa kwao Mwenyezi Mungu, na kuikanusha Akhera na kukamia juu ya waliyoyakuta kwa wazee wao. Wakabainishiwa ubatilifu wa haya kwa hoja zilizo dhahiri, zinazoingia mabongoni mwao zikaathiri katika nyoyo zao. Wakaondoshewa kila kitakataka cha shaka waliyokuwa nayo juu ya ukweli wa ulingano huu, na wakajibiwa kila hoja zao kwa hoja za kweli kweli na mfungulio usiokuwa na

chembe ya fundo wala tanzi juu ya hayo waliyokuwa wakiona yanawatanza, au wakitaka tu kuwatanzishia wenzi wao. Al muradi ukafiri ulitiwa mbaroni barabara, kila upande ukawa umezingiwa, pumzi hauna, hata ukatolewa maanani. Na juu ya hivi wakaonywa, kwa ghadhabu ya Mwenyezi Mungu na vituko vya Kiyama na adhabu ya Jahanamu. Na wakatahayarishwa kwa zile tabia mbovu walizokuwa nazo, na mwendo ulio batili na ada za Kijahili na kuipinga hii dini japokuwa wanaijua, na kuudhi Waislamu. Wakaonyeshwa misingi ya Akhlaqi nzuri na ya Ustaarabu ambao kwa Ustaarabu huo ndio ilipatikana tamaduni iliyoenea ulimwengu mzima na ikapata radhi ya Mwenyezi Mungu. Sehemu hii ilikuwa na vipembe vyake vingine vidogo vidogo. Basi kwa vipembe hivyo ukawa unasonga mbele tu ulingano huu wa Uislam, na ugomvi wa makafiri unashtadi na moto wao unazidi kuwaka. Na kila siku ukawa ulingano huu unaletewa Itiqadi mpya mpya na unakabiliana na maadui wapya wapya. Na Aya za Qurani zikazidi kuleta namna namna za misemo na madhihirisho ya mambo yake. Basi hii tarikhi ya mteremko wa Qurani kwa Aya zake zilizoteremka Makka.

Muda huu ulichukua miaka kumi na tatu — mpingano mkubwa kabisa. Kisha ulingano huu ukapata matulio yake Madina. Ukaweza sasa kuweta watu wake waliokuwa katika kila kipembe katika vipembe vya Bara Arabu. Wakajiweka katika kichungu kimoja na wakazikusanya nguvu zao zote pamoja. Basi akahajiri Mtue na sehemu kubwa kabisa ya watu wake, wakaja Madina. Sasa Ulingano wa Uislamu ukaingia katika daraja yake ya tatu.

Mambo yakageuka chini juu. Uislamu ukaweza kuweka msingi wa dola kamili yenye kujitosha wenyewe.

Sasa vikaanza vita vya Silaha za kuua, si vita vya silaha za maneno.

Sasa vile vile ukakabiliana Uislamu na uma zilizokuwa zikifuata Mitume iliyotangulia — Mayahudi na Manasara — kama ulivyoingia kukabiliana na wanafiki waliojitia katika hiki kikundi cha Uislamu. Na baada ya taabu kabisa na mgongano mrefu kabisa wa miaka kumi, Uislamu ulifikilia upeo wa nguvu zake na uweza wake na ufalme wake; wakadhili Waarabu wote chini yake na wakanyenyekea na ikafunguka milango ya kutangaza ulingano wake ulimwengu mzima na kusimama kuleta matengenezo yaliyoenea kila mahala. Na hii daraja ya tatu ina vipembevipembe vyake, umetekeleza Ulingano wa Uislamu katika vipembe hivyo yaliyokuwa yakihitajiwa. Na kwa ajili ya kutekeleza hoja hizo Mwenyezi Mungu akateremsha Qurani kwa mnasaba wa hoja hizo na mambo hayo. Mara husema kwa ukali unaotoa macheche ya moto, na mara kwa msemo wa maamirisho ya kifalme, na mara kwa msemo wa kialimu, na mara kwa msemo wa mtoa mawaidha, mwenye nasaha na mwongozi wa kweli. Ikabainishwa katika Qurani namna ya kufanya uma, namna ya kufanya dola na namna ya kufanya na kutangaza Ustaarabu, na namna gani yanasimamishwa mambo mengine na kuendeshwa. Na ikafundishwa namna gani kukaa na wanafiki, kukaa na wasiokuwa Waislamu, na namna gani kuwaendesha hawa walioamini ili wasimame kuuendesha ulimwengu wote. Aya hizi za sasa zikiteremshwa katika kuwaongoza Waislamu na kuwachunga vizuri, na kuwazindua wanapotaka kuteleza, na zikiwahimiza sana sana kutoa roho zao na mali zao katika kuipigania dini; na zikawapa masomo barabara katika Akhlaqi nzuri na vipi kukaa na viumbe na kuwasarifu. Aya hizo zikinasibiana na vile kushindwa kwao katika vita au kushinda, na balaa na raha, na kheri na shari na amani na khofu na yaliyo kama haya. Na walikuwa wanafanyika watu wa kweli kweli wa kuweza kuja kumpokea Mtume atakapoondoka na wafuate mwendo wake katika hima na uzuri wa kutangaza Ulingano huu. Na vile vile Aya hizo zikawalingania watu wote wa kila namna. Wasioukubali Uislamu, zikawalingania kufuata kheri hii na haki hii, kwa mnasaba wa hali ya kila mmoja katika hao na mnasaba wa kisimamo

chake katika kuupinga Uislamu. Wakilinganiwa kwa hoja zilizo na nguvu kweli kweli na maneno laini na kwa mawaidha mazuri na kusimangwa na kukhofishwa adhabu ya Mwenyezi Mungu. Wakitakiwa wazingatie kila upande kwa yaliyopita na yanayopita. Ipate kukamilia hoja juu yao na wasiwe na udhuru tena. Na huu ndio mwendo wa Qurani baada ya kuhamia Mtume Madina.

Basi imebainika kwa haya tuliyoyataja hapa kuwa mteremko wa Qurani ulikuwa umekamatana na ulingano wake na daraja za mwendo wake. Vikiteremka vipande mbali mbali kwa nyakati mbali mbali na kwa haja zinazozukia katika kila mapitio ya Ulingano huo unavyopitia, tangu mwanzo wake mpaka kukamilika kwake kabisa kabisa. Na umechukua kiasi cha miaka ishirini na tatu. Na hapana shaka kuwa mwandikaji wa jambo namna hii inamlazimikia afuate namna ile anayofuata mwanafunzi wa Ma-University wakati anapojitegeneza kwa ajili ya kupata Ma-degree yake. Na hivyo vipande vya Qurani vilivyokuwa vikiteremka kidogo kidogo havikuwa vikiandikiwa katika sura ya vitabu wala vipamphlet; bali vilikuwa vikisemwa tu hivi, kama khutuba na Vikipokewa kwa midomo tu na kuhifadhiwa vifuani. Na vilikuwa haviteremshwi kwa msemo wa vitabu bali kwa msemo wa khutuba ambazo hazishabihi khutuba za walimu wa Ma-University, bali khutuba za mlingani anayetaka kuleta hamasa za wasikizi wake na kuzisisimsha akili zao na nyoyo zao; si hamasa tupu. Kwa hivyo kila watu ikawasemeza kwa kiasi cha akili zao na kwa kiasi cha taathira ya ule ulingano wake kwao kwa nyakati mbali mbali na hali zilizokhitalifiana. Inataka kuuthibitisha ule ulingano ndani ya nyoyo zao hao watu, kutengeneza namna ya kuthibitisha hivyo, kuchemsha nyoyo zao, kuvunja nguvu za ushindani wao, kuwatengeneza wafuasi, na kuvuta hamasa yao, kuwabadilisha wawe marafiki wa kweli kweli, kuwapelekea wakanyaji wakiri — kwa dalili wanazoonyeshwa — kuvunja hoja za hao wanaopinga na kuondosha uwongozi wao mwovu. Na yaliyo kama haya ambayo yanampasa Mwongozi ayafanye akitaka uwongozi wake ufanikiwe. Na kwa kutazama haya basi Sura na Aya zilizokuwa zikiteremka wakati huu kwa jambo hili zilikuwa kwa maneno na mpango wa kikhutuba, kwa namna ya kuathiri kweli kweli na kunasibu ile hali waliyokuwa nayo wakati huo. Kwa hivi hazitakuwa — kama wanavyotaka watu wa sasa ziwe — zinashabihi khutuba za makhatibu wa Ma-*University.*

Kwa hivi imekubainikia dhahiri sasa siri ya kutakarari maneno ya Qurani, kwani hivi ndivyo inavyotakikana kwa kuchunga kila wakati wa zile nyakati mbali mbali zilizopitiwa na Ulingano huu kama tulivyoona. Katika kila wakati ilipasa yakaririwe barabara juu yao hayo yanayotakikana waambiwe. Basi ndio maana yakakaririwa hivyo. Lakini yakikaririwa kwa alfadhi mbali mbali na mpango mbali mbali unaoshawikisha kuusoma na kuusikiliza, ili nyoyo zione raha na masikio na akili pia zifurahike. Na katika daraja zote hizi mbali mbali yanaletwa mara kwa mara yale ambayo yalikuwa ndio msingi khasa wa Uislamu tangu hapo mbele kabisa. Ndiyo maana katika kila daraja unayokuta baadhi ya haya: Mambo ya Tawhidi na Sifa za Mwenyezi Mungu na Masuulia ya mwanaadamu na mambo ya Akhera (neema zake na ikabu zake), na habari za Utume na kuamini maneno ya Mungu na kucha Mungu na kusubiri na kuvumilia na kumtegemea Mwenyezi Mungu na yaliyo kama haya; haya yamekaririwa katika Sura za Makka na za Madina. Kwani Ulingano wa Uislamu hausuluhii pasi na kuyakumbusha haya. Na lau yangepuzwa haya, Uislamu usingekwenda mbele kwa namna inayotakiwa.

Ukisha kuyajua haya utapata Jawabu ya Suala hili: Kwa nini Mtume asizipange Aya za Qurani kwa mnasaba wa kuteremshwa kwake.

Tumeona kuwa Qurani imeteremshwa kwa mnasaba wa daraja uliyoifikia ule Ulingano wa dini ya Uislamu katika kupanda kwake. Basi ikawa sio mpango wa kupendeza kuipanga kwa mnasaba wa kuteremka kwake. Mpango muwafaka ni huu wa kuweka kila yanayonasibiana yawe pamoja japokuwa hayakuteremka wakati mmoja. Hapo mwanzo walikuwa wanasemeshwa watu wajinga kabisa, hawajui lo lote lile la Uislamu, wakawa wanatupiwa kidogo kidogo yale ya kuwazindua kuiendea Imani na taalimu. Sasa ilivyokuwa Uislamu umekwisha kujikusanya pamoja na yamekamilika mambo yake, na Waislamu wamekwisha kuwa uma kamili wa kuongoza ulimwengu, imekuwa wapangiwe mpango huu wa kuwaonyesha wajibu wao na njia za kuendeshea dunia yao na Akhera yao na kuwahadharisha na misukosuko na maradhi yaliyosibu uma nyinginezo za Mitume waliotangulia. Yawaelee haya vyema kabla ya kusimama wao kuongoza ulimwengu wote mzima — ulimwengu ambao ulikuwa umepotea kabisa.

Mtu aliyewafikiwa hidaya ya kuijua Qurani ataona kuwa mpango huu ndio muwafaka. Sio kuweka za Makka mbali na Madina mbali. Muwafaka ni hivi kuchanganyika. Anazisoma za Makka wakati huo huo anapozisoma na za Madina. Na kinyume chake. Na anayasoma yale yaliyoletwa mwanzo, pale pale anapoyasoma yaliyoletwa mwisho, aone Uislamu ulivyopangika kwa uzuri usiokuwa na mfano na kwa mpango hakuna mwengine ulio ndio kuliko huo.

Lau ingepangwa Qurani kwa mpango wa kuteremka kwake usingeleta faida hii ya mpango huu. Na ingetaka itiwe tarikhi za kuteremka Aya zake na sababu ya kuteremshwa kwake. Na haya yangekuwa mambo ya kupachikia katika Qurani. Na Mwenyezi Mungu anataka kitabu chake kiwe kimesafika na kupachikiwa maneno ya watu. Yawe maneno Yake peke yake, hayakuchanganyika hata chembe na maneno ya viumbe. Yawe maneno yake tu Mwenyewe Muumba, katuletea ya kutuongoza sisi aliyetuumba. Kwani hakuna anayejua ya kutufaa kuliko Yeye. Kwa mpango huu anapata faida kwa Qurani, mwanamume na mwanamke, mpevu na mchanga, mkubwa na mdogo, mwanachuoni na asiyekuwa mwananchuoni, na jalimu la kweli kweli pia, wakazi wa mijini na wa mashamba na majangwani; wa kila zama na kila mahala, na katika kila hali. Na wajue watu wote — wenye kukhitalifu katika daraja za akili na mengineyo — wajue wote nini alichowatakia Mwenyezi Mungu wakikue. Siyo kuwatilia na maneno ya viumbe.

Hapana shaka kuwa hao wanaoupinga mpango huu wa Qurani wanataka kipangwe kitabu hiki cha uwongozi wa Mwenyezi Mungu kama vinavyopangwa vitabu vya Historia na *Welfare* na kama haya.

Na mpango huu wa Qurani hawakuupanga waliokuja baada ya Mtume. Ni mpango aliojulishwa Mtume na Jibril kwa amri yake Mwenyewe Mwenyezi Mungu. Mtume alikuwa na waandishi wake makhususi wa kuandika Aya za Qurani kila zinapoteremka au vipande vya Aya. Ikiteremka Aya fulani au kipande chake mara Mtume anawaambia: 'Aya hii (au kipande hiki) iwekeni ubavuni mwa Aya fulani iliyoko katika Sura fulani''. Na Mtume huwa kafundishwa na Jibril kufanya hivyo kwa amri ya Mwenyezi Mungu. Na ikimalizika Sura vile vile anawambia kuwa Sura hii imekwisha kukamilika haitaongezewa tena kitu na iwekwe baada ya Sura fulani. Na Mtume na Masahaba tangu siku hizo wakiisoma Qurani — katika Sala na penginepo — kwa mpango huu wanousoma Waislamu mpaka leo. Hao Masahaba waliohifadhi Qurani zama za Mtume na baadaye — na kila walioihifadhi Qurani tangu zama za Mtume na baadaye — na kila walioihifadhi Qurani tangu zama hizo mpaka leo — wameihifadhi namna hii iliyomo ndani ya Misahafu hii waliyo nayo Waislamu wote; na ndivyo

ilivyokuwa kaihifadhi mwenyewe Mtume. Na tangu ilipoanza kuteremka ilianza Kuandikwa na Kuhifadhiwa na Kusomwa kila mahala. Katika kila jambo ikisomwa Qurani. Ikiandikwa katika karatasi za wakati huo. Nayo ni Mapongoo ya mitende, ngozi za wanyama zilizotegenezwa, vidifu (fupa pana la bega) vya wanayama na kama haya. Ikihifadhiwa Qurani katika vifua vya mamilioni ya Waislamu tangu siku hizo mpaka leo.

Alipokufa Mtume kilitokea kishindo kikubwa; cha kurtaddi (kuwacha watu dini ya Uislamu) na kupigana na Waislamu wasioritadi. Wakafa Masahaba wengi kabisa. Na wengi katika hao walikuwa katika wale chungu ya Masahaba waliokuwa wamehifadhi Qurani. Hapo Sayyidna Umar akatoa rai ya kuandikwa Qurani yote nzima mahala pamoja. Akaishadidia rai yake hii mpaka ikakubaliwa na kuwafikiwa na watu wote. Na hapo Khalifa — Sayyidnna Abubakr — akaamrisha ikusanywe yote pahala pamoja badili ya kuwa sehemu nyingine imo katika mifupa, nyingine katika ngozi na nyingine katika mapongoo. Uraisi wa kazi hii aliwachiwa Bwana hodari kabisa, Bwana Zaid bin Thabit, ambaye ndiye aliyekuwa raisi wa waandikaji hii Qurani zama za mwenyewe Mtume. Yalikusanywa maandishi yote yale ya Qurani nzima yaliyoandikwa yakawa kwa Mtume. Yakalinganishwa na maandishi ya kila Sahaba aliyepata kuandika, na yakalinganishwa na Hifdhi za wale waliohifadhi Qurani. Na walikuwa wengi. Ukaandikwa Msahafu mmoja madhubuti barabara uliokabilishwa kwa zote hizo njia tatu. Msahafu huo ukawa katika Hifdhi ya Sayyidna Abubakr. Na anayetaka kunakili ananakili. Alipokufa Sayyidna Abubakr ukawa katika Hifdhi ya Khalaifa wa Pili — Sayyidna Umar. Na wanaotaka kunakili wananakili. Alipokufa ukawa kwa mwanawe mwanamke, mkewe Mtume — Bibi Hafsa. Na anayetaka anakwenda kunakili.

Waarabu wenyewe kwa wenyewe walikuwa wanakhitalifiana — kidogo au sana — katika matamko yao ya Kiarabu na maneno yao, kwa mnasaba wa kubaidika kwa mahala pao wenyewe kwa wenyewe, kama hivi kinavyokhitalifu Kiswahili cha Kiunguja na Kimombasa na Kilamu na kama hivi. Bali wao wakikhitalifiana zaidi, kwani masafa ya nchi yao yalikuwa makubwa zaidi. Basi hapo mwanzo wa Uislamu walipewa ruhusa kuitamka Qurani kwa muwafaka wa matamshi ya mwahala mwao humo, japokuwa tafauti kidogo na lugha fasihi kabisa, lugha ya Kiqureshi — lugha yake Mtume — ambayo ndiyo ikiteremka hii Qurani kwa lafdhi zao; khalafu Mtume anawatamkia hao wengine kwa matamshi ya kikwao ambayo yote Mtume akiyajua, na akiwasemesha kwa matamshi yao hayo wakati mwengine. Na maana ilikuwa ile ile moja.

Khalafu Uislamu ulipotangaa kila mahala, na Waislamu wa huku na huku — katika Bara Arabu na kwingineko — wakawa wamechanganyika sana sana na kuingiliana kukubwa sana, ilionekana bora utangazwe ule Msahafu wa Mtume ulioandikwa zama za Sayyidna Abubakr. Zipelekwe Nuskha (copy) zake ulimwengu mzima wa Kiislamu wa zama hizo. Haya aliyafanya Sayyidna Uthman bin Affan katika zama zake, kwa rai yake na Masahaba wenzake wote. Basi akachaguliwa yule yule Sayyidna Zaid bin Thabit — na akaongezewa na wengine — waunakili ule Msahafu ulioandikwa zama za Sayyidna Abubakr ulionakiliwa kwenye maandishi aliyoamrisha Mtume na ukaandikwa kwa lugha ya Mtume — lugha ya Makureshi. Zikaandikwa nuskha (copy) nyingi.

Nuskha nyingine zikapelekwa Makka (Hijaz), nyingine Damashq (Damascus — Sham), nyingine Al Kufa (Iraq), nyingine Al Basra (Kusini ya Iraq), nyingine Yaman. Na nyingine zikawako Madina. Wakaamrishwa kila wanaotaka kuandika Qurani wanakili katika nuskha hizo, waache hizo nuskha zao zilizoandikwa kwa lugha zao.

Basi hii Misahafu yote iliyoko ulimwenguni sasa — ambayo yote ni ya namna moja —

ni nuskha ya huo Msahafu wa asili kabisa ulioandikwa zama za Sayyidna Abubakr. Na zinapatikana bado katika Mamuseum baadhi ya hizo nuskha za asili. Na msahafu wa nchi yo yote ile ya Kiislamu ukiupeleka nchi nyingine, japokuwa iko mbali kabisa na hapo, utauona sawa sawa na hiyo ya huko. Na Misahafu ya kila karne — tangu hiyo karne ya Mtume — utaiona sawa sawa. Akiweza mtu kuona tafauti naatangaze Uvumbuwaji wake huo wa ajabu katika mambo ya Tarikhi. Anayetaka kujitia shaka haitiliki hapa. Ni kama hivi tulivyosema. Naauonyeshe Msahafu huo uliotafautika na Misahafu myenziwe (mengine). Kujitia shaka katika jambo hili ni kama kujitia shaka kuwa jua halitoke ulimwenguni. Na hiyo ndiyo shaka inayoonyesha wazimu.

Na hii Qurani inasomwa na chungu nzima kabisa ya watu kwa makusudio mbali mbali. Kwa hivi siwezi kutoa fikra zangu kuwapa hao wasomaji kwani makusudio yao ni mbali mbali. Lakini nawapa fikra zangu wale wanaoisoma kwa kutaka kuifahamu na kujua uongozi wake katika mambo ya dunia na Akhera. Hawa napenda kuwafungulia mishikili yao inayoweza kutokea.

Kwanza inampasa huyo anayeisoma hii Qurani — akiwa Mwislamu au si Mwislamu — asafishe akili yake na yaliyo ndani ya fikra yake hiyo ya itikadi zake na mawazo yake ya kuipenda au kuichukia. Sasa azame barabara katika kuisoma kwa moyo wazi na sikio kali na makusudio safi ya kutaka kuifahamu. Ama wale ambao wamekwisha kutia katika nyoyo zao fikra makhsusi juu ya Qurani na Uislamu, basi hata watakapokuwa wanaisoma hiyo Qurani itakuwa wanawaza kwa hizo fikra zao walizo nazo, wasiijue hakika ya Qurani. Bali kitabu cho chote kile akikisoma mtu kwa yaliyo katika fikra zake atakuwa amegandwa na zizo hizo fikra zake, hatakipatia faida.

Ama yule anayeisoma Qurani aijue vivi hivi tu juu juu, basi inamtosha kusoma mara moja mbili. Ama anayetaka kuisoma khasa, hata mara tano hazimtoshi. Inataka aisome mara kwa mara kwa dhati yake na bila ya kuchoshwa na kutoshwa. Na kila mara aizingatie kwa namna nyingine. Tena afanye — kama wanavyofanya watoto wenye hima wa Ma-*University* — awe na *Note-book* yake na kalamu yake ya kuandika kila analoona hili muhimu au geni, linataka kudhibitiwa. Na vile vile ikimjia raghba ya kuuliza asiulize, bali aiandike suala yake. Hatamaliza kuisoma Qurani ila atapata mumo humo jawabu yake. Na kama hakuipata hiyo jawabu yake katika kuisoma mara ya kwanza naisome tena mara ya pili kwa subira na ustahamilivu; ataipata tu. Na kama palikuwa na la kumtatiza litatanzuka tu, ila kwa nadra kabisa.

Kuisoma juu juu ndiyo kama hivi tulivyosema. Ama akitaka kuisoma vilivyo khasa, nakidhibiti kila anachokipitia; kama vile kudhibiti sifa zote ambazo Qurani inasema kuwa ndizo sifa ambazo kila mtu inataka asifike nazo. Na vile vile kudhibiti sifa zote ambazo Qurani inataka mtu ajiepushe nazo. Azilinganishe barabara hizi na hizi. Na adhibiti kadhalika mambo ambayo Qurani inasema kuwa kwa mambo hayo ndiyo kunapatikana kufanikiwa (ufanikio), na kwa mambo hayo mengine ndiyo kunapatikana kuharibikiwa. Na awakumbuke waliotengenekewa kwa hayo na walioharibikiwa kwa hayo. Na kila mengine yote yanayotajwa katika Qurani ayadhibiti hivi na kama hivi; lakini ayadhibiti, yasiwe yanaingia sikio hili yakatoka sikio la pili.

Na akitaka kujua nini fikra za Qurani katika jambo makhsusi hivi lililo muhimu, nasome kwanza nini fikra za wasiokuwa Waislamu kwa jambo hilo na rai zao walizotoa — wa zamani na wa sasa — na yepi waliyoyataja na yepi wasiyoyataja. Halafu aisome Qurani, ataona namna gani rai nzuri ya Qurani juu ya mushkili huo ambayo hakudhani kuwa ataipata.

Na juu ya jitihada yake yote ya kila namna hawezi kufikilia khasa kiini cha Qurani na hakika yake maadamu hatayafuata khasa yaliyomo humo kama yalivyo. Qurani si kitabu cha kusoma tu — juu ya kiti chako — ukatazama nini fikra zake kama vitabu vyingine. Wala si kitabu cha kunga na mambo ya siri ambayo hazifichuliwi kunga zake ila mahala makhsusi. Hii Qurani ni kitabu cha kulingania haki na kuifuata, kwa vitendo, si kwa maneno matupu.

Mungu alimteremshia mtu mpole kabisa, mwenye tabia nzuri mno kabisa, na moyo safi kabisa, wala simropokwaji wa maneno ya upuzi. Akamwamrisha aukabili ulimwengu mzima ambao wote ulikuwa umetupa haki; apigane na batili yao hiyo aiondoshe. Kikapokewa kitabu hiki na kila roho nzuri na nafsi katika kila nyumba. Wote hao wakakusanyika chini ya bendera ya Mtume. Na kikamwudhi kitabu hiki kila aliyekuwa fisadi mharibuji, akaingia kuwapinga na kuwapiga wale waliokipokea. Kitabu hiki ndicho kilichosimamisha Mwendo wa Uislamu mkubwa huo muda wa miaka ishirini na tatu, ulioanza kwa ukelele wa mtu mmoja tu, ukenda mpaka ukaonyesha utawala wa Kimungu ulimwengu mzima, ukavunja batili ikavunjika, ukajenga haki ikaamirika. Vipi itaweza kukudhihirikia wewe siri yake mara moja kwa kupitisha tu harufu zake katika kinywa chako? Sharti yakupitie hayo yaliyowapitia hao waliokikubali huko mwanzoni, wakayakabili kwa kifua cha nguvu yote hayo yaliyowakabili — mitihani na misukosuko na vita: Badr, Uhud, Khaybar, Makka, Taif, Tabuk na kwengineko. Upambane na mifano ya hiyo mikafiri mikubwa kama kina Abu Jahl na Abu Lahb, na wanafiki wazandiki, na Mayahudi wenye namna namna za viroja. Hii ni safari ndefu ya kwenda na Qurani. Na kila ukifika kwenye kituo kimoja utakutana na Sura na Aya za Qurani za kukufidisha materemko yake katika uwongozi wa Qurani. Hapo Qurani haikufanyii ubakhili kukufunulia hakika yake khasa. Basi maadam mtu hakuifuata khasa — khatwa khatwa — hii Qurani, hataweza kuijua khasa ilivyo, akiwa mtu mmoja au uma mzima. Maadam wanakwenda kinyume na mwendo wa Qurani basi hawawezi kuijua ilivyo.

Na kila mtu anajua kuwa Qurani imekuja kuwaongoza Binadam wote. Lakini anapoisoma mtu huona kuwa haiwasemezi ila Waarabu waliokuwa zama hizo, japokuwa wakati mwengine imewageukia na watu wengine. Lakini mahala pengi ataiona inasemeza dhauku ya Waarabu na mwendo wao na tarikhi zao na maisha yao. Ikiwa Qurani imeteremshwa kuongoa wanaadamu wote kwa nini kwa muda mrefu inawasemeza watu makhsusi — kuhusu mahala pao na tarikhi zao na nyendo zao? Basi huenda akatia shaka mtu akasema — "Naona' mimi hii Qurani imeteremka kuwatengeneza hao Waarabu waliokuwa zama za Mtume; kisha Waislamu waliokuja baadaye ndio walioinasibishia (hii Qurani) kuwa imeteremshwa kuongoza binaadamu wote na kwa zama zote mpaka Kiama".

Akisema mtu hivi tutambwambia — maadamu si mwenye inda na na ubishi — "Tuonyeshe Aya moja inayoamrisha mema au inayokataza mabaya au inayohimiza au kukosoa au kulaumu au. . . Ukaiona kusa hii haiwasuluhii ila Waarabu tu, tena waliokuwa katika zama hizo za Nabii Muhammad." Hataiona Aya namna hiyo. Alama kuwa kutajwa hayo ya Waarabu na ya waliokuwa Muhammad." Hataiona Aya namna hiyo. Alama kuwa kutajwa hayo ya Waarabu na ya waliokuwa karibu nao ni mfano tu ya kutolea dalili, siyo ya kuonyesha kuwa hayo yanayosemwa yamewahusu wao tu. Sasa Inshallah imetubainikia vizuri kuwa hizo ni stishhadi tu. Tazama Qurani — mathalan — inapovunja ushirikina ikathibitisha Tawhid, hoja hizo si zinasuluhia kuvunja ushirikina wa kila washirikina au washirikina wa Kiarabu tu? Ataona zinasuluhia kwa kila ushirikina. Na vile vile hoja zake na dalili zake katika kuthibitisha mazuri mengine na kubatilisha mabaya mengine, si zinasilihi kwa kila Wanaadamu wa kila wakati na wa kila mahala? Ataona ndio zinasilihi kwa kila wanaadamu

wa kila zama na kila mahala. Basi kwa nini atasema mtu kuwa Qurani imewahusu Waarabu wa zama za Mtume tu basi? Hapana madhehebu yoyote yanayoitia watu wowote kwenye jambo lolote lile, yakasema maneno yake vivi hivi tu bila ya kutoa mifano ya mambo yaliyo karibu na hao waanzaji wake. Haimkiniki kutangaza uwongozi (uitaji) bila ya kuutolea mifano ya karibu kwanza. Na kama uwitaji fulani utaitia watu kwenye uitaji bila ya mifano basi utakufa njiani, yasalie maneno juu ya karatasi tu.

Na ulingano unaotaka utapakae ulimwengu mzima si lazima kuwa tangu mwanzo kabisa uanzie hivyo. Lakini njia nzuri ni kuanza kwa yale ya karibu na walio karibu; ukawa unatoka nje kidogo kidogo, kama duara ya maji inayoanza kwa kutupa jiwe — inapanuka na kupanuka na kupanuka mpaka linakuwa duara kubwa kabisa, limefikilia mwisho wake. Basi ndiyo hivyo; uwaonyeshe watu wa karibu yako namna ulivyowaongoa, kisha waliofuatia hapo, tena waliofuatia hapo, mpaka ifike khatima yake. Taratibu ndio mwendo. Yakianzwa mambo namna hii ndipo yanapovuta uma nyingine upesi upesi, kwani huwa zimekwisha kuona natija nzuri ya ulingano huo. Sio kurukia mara moja bila kuonyesha dalili ya kuwatengeneza wa karibu yako, ukaonekana uwongozi wako.

Basi kule kuanzia jambo kwa watu makhsusi kwanza, ukapitisha kila jitihada zako katika kuwabainishia kwa kila hoja na dalili ili wakinai barabara kwa hoja hizo na wafuate, siyo dalili ya kuonyesha kuwa jambo hili limewahusu watu hao tu. Alama ya kuonyesha kuwa jambo hilo limehusishwa kwa watu makhsusi tu ni hii: Jambo lililohusishwa kwa watu makhsusi huwafadhilisha watu hao kuliko wengineo, na huwatakia haki lisizowatakia wengineo, na huleta mambo ambayo hayamkiniki kukubaliwa na wengineo. Na kinyume cha jambo lililokusudiwa liwe la watu wa ulimwengu wote. Jambo hili huwafanya watu wote sawa sawa, likawapa wote haki moja kwa daraja sawa sawa, na mambo yake yote yakawa ya kuwafiki ulimwengu mzima. Na jambo la kukusudiwa wakati makhsusi tu, huleta mambo yake kwa namna ambayo hayasilihi ila kwa wakati makhsusi tu. Kinyume cha jambo lililokusudiwa umilele. Jambo hilo mambo yake yote huwa yanapigia yawe ya umilele na maisha, na kufaa katika hali zozote zile, zitakazokuja na zitakazokuwa. Basi yuko yoyote yule aliyeisoma Qurani, au atakayeisoma, akaiona mna jambo lake humo — japokuwa moja — la kuonyesha la kufaa katika wakati makhsusi tu au la kufaa watu makhsusi tu? Hayuko wala Hakuwapo wala Hatakuwapo mtu huyo.

Na katika wenye kukisoma kitabu hiki, kuna ambao wametia katika nyoyo zao kuwa kitabu hiki ni cha kutaja mambo na dasturi kwa kuyachambua moja moja, kwa wingi wake na uchache wake na kwa utungo wake. Lakini anapokisoma hakioni hivi. Bali ataona hata hayo mambo muhimu kabisa kama Sala na Zakaa ambayo yanatajwa mara kwa mara na kushadidishwa sana, hatayaona yamepangwa hivi. Basi hapo itashawishika akili yake aseme "Basi vipi kitabu hiki kinaambiwa ni Uwongozi unaotoka kwa Mwenyezi Mungu?"

Basi tashwishi hii humfika yule ambaye haikumpitia katika akili yake kuwa:- "Mwenyezi Mungu hakukileta kitabu chake hiki kitupu, hayuko wa kuwaongozea watu." Mungu kakileta pamoja na Mtume Wake. Yeye aendeshe namna inavyotakiwa kuyaendesha yanayotakiwa, mpaka yawe yanavyotakiwa. Jengo lisimame linavyotakiwa. Na huyo Mtume wake amemtengeneza kweli kweli awe mjenzi asiyezidiwa. Hapikuliwi na yoyote kwa chochote. Basi kwa hivi imekuwa si lazima kubainishwa kimoja kimoja na mpango wake hata mdogo wake na mdigi wake, kisiwache kibainishwa hata kidogo chake na kidigi chake. Hapakuwa na haja ya haya. Na ulimwengu mzima umeona namna alivyolisimamisha jengo zuri imara hilo lililokusudiwa. Basi Qurani si kitabu cha kubainisha mambo madogo na

madigi. Bali ni kitabu cha kutaja Misingi ya mambo na Nguzo zake na Mihimili yake — Kuyataja hayo kwa ubainifu na kwa namna ambayo yatathibiti barabara kwa dalili za akili na za kuingia katika nyoyo. Qurani imeweka mipaka mine ya kila mbinu katika mbinu za uhai, kwa muwafaka wa mpango wa kumridhisha Mwenyezi Mungu. Na kazi ya Mtume ilikuwa auongoze mwendo wa Kiislamu kwa muwafaka wa haya yaliyotajwa katika Qurani. Hakuletwa Mtume ila awe ndiyo ruwaza ya kuonyesha ulimwengu wote mzima kuwa Mwislamu anayefuata Qurani huwa hivi, na dola inayoendeshwa kwa kufuata Qurani huwa hivi. Na yamepatikana haya, chapa kwa ya pili.

Na hapa pana suala jingine, nalo ni hili: Qurani imewalaumu na kuwakamia kweli kweli wenye kukhitalifiana baada ya kujiwa na uwongozi wa Mwenyezi Mungu, wakafarikiana mbali mbali. Basi mbona wamekhitalifiana Waislamu katika tafsiri ya baadhi ya hukumu za Qurani, bali na katika tafsiri yake — tangu hao Masahaba na Matabiina na Maimamu na waliokuja baada yao? Takriba huwezi kupata Aya yoyote isiyofanyiwa khitilafu. Basi Waislamu hawa hawastahiki kulaumiwa? Khitilafu gani nyingine isiyokuwa hii inayoharimishwa na Qurani na kuchukiwa?

Mwenye Suala namna hii kwa ufupi tutamjibu hivi. Uislamu haulaumu khitilafu inayopatikana kwa njia safi ya kutengeneza, kama hiyo waliyoipita hao waliokhitalifiana katika kufasiri lafdhi au hukumu au kanuni zilizokamatana na Qurani, maadam wote wanakutana pale pale penye msingi mmoja na mtengenezo mmoja, wa kuutengenezea uma wa Kiislamu. Khitilafu inayotukanwa na Uislamu ni ile khitilafu inayopatikana kwa nia mbovu ya kuharibu na ya kufarikisha watu wenyewe kwa wenyewe, wawe wa vichungu mbali mbali, na kila kimoja kinavutia upande wake bila ya kutafuta haki, ila chuki tu na inadi. Basi khitilafu ni namna mbili kama unavyoona hapa, na natija zao mbali mbali. Basi vipi unazipa hukumu moja? Ile khitilafu ya kwanza inayopatikana kwa jitihada na kukhitalifu fikira na ilimu, hiyo ni khitilafu inayoonyesha kupanda watu na kuzidi ilimu yao na kusitawi katika uhai wao, sio kufa. Na khitilafu hii lazima ipatikane katika kila uma wa watu wanaoienzi akili na fikira na rai; nayo ndiyo dalili ya uhai wa uma huo. Na lazima ipatikane katika kila ungamano la watu wenye akili na utambuzi na huria ya kusema. Ama ile khitilafu inayokuja kwa ajili ya kuleta khitilafu tu au kutengana, haipatikani ila huutawanya uma huo mbali mbali na ukaubaraganya vibaya. Kudhihiri khitilafu hii ni alama ya ugonjwa wa uma huo, kinyume cha kudhihiri khitilafu ile. Ile ni alama ya uhai wa uma huo na siha yake nzuri.

Na mfano wa khitilafu mbili hizi ni hii. Katika ile khitilafu nzuri iliyopatikana katika Uislamu ni kuwa wote hao waliokhitalifiana wametafikiana juu ya mambo namna haya. Kumtii Mwenyezi Mungu na Mtumewe. Kuitikadi kuwa Qurani na Hadithi ndio msingi wa kutolea Hukumu na Sharia. Na wakikhitalifu Maimamu wawili au makadhi wawili, kila mmoja haoni kuwa rai yake na mas-ala aliyokhitalifu na mwenzake, ndiyo nguzo ya dini na akamfanya mwenziwe aliyemkhalifu kuwa ni mkhalifu wa dini. Bali kila mmoja huitolea rai yake hoja kamili na shabaha za haki, kisha akawawacha wenyewe watu watazame la kufuata katika hizo rai mbili na zaidi au wafuate zote. Na hivi ndivyo yalivyo madhehebu ya Kiislamu yaliyo madhehebu ya Kiislamu kweli.

Na katika ile khitilafu mbaya ya kudhuru ni kuwa ile khitilafu imo kwenye msingi wa dini na nguzo zake. Au kukhitari mwanachuoni wa Fiqh au wa Tasawuf au mufti au muongozi yoyote au mkaidi yoyote — akakhitari — rai yake katika ma-sala ambayo Mwenyezi Mungu wala Mtume wake hawakuyafanya kuwa ni ya msingi wa dini, akayafanya yeye — kwa migeuzogeuzo yake na mipachiko yake — kuwa ni mas-ala ya dini na

akamhukumia ukafiri kila anayemkhalifu, na akafanya kikundi chake na kusema kwa kinywa kipana: "Uma Muslim ni huu, na asiyekuwamo humu ni wa Motoni." Na akanadi tena: "Ingia katika kikundi hiki kama wewe Mwislamu kweli, na kama huingii basi si Mwislamu". Basi khitilafu inayochukiwa ni kama hii. Ama ile ya awali ilitokea hata zama za Mtume, na Mtume akaikiri na kufurahi nayo. kwani ilikuwa inabashiri na kuonyesha kuwa uma huu una fahamu na fikira na kuzingatia na kupima na kuwaza na kuwazua na kutafuta lililo ndilo na lenye maslaha, na kuwa wana hima ya dini yao na kuwa wanachukua yao katika dini yao si nje ya dini yao. Na uma unaokamata rai hii ya kuwa wajitahidi, lakini wasitoke na msingi na nguzo za dini yao, ili wawe pamoja na wawape fursa wenye akili kubwa safi na ilimu kubwa safi, na rai nzuri safi, na wenye . . . watumie jitihada zao katika kutafuta na kuhakikisha, bila ya kutoka nje ya mipaka ya dini, uma huu unastahiki kuandikwa habari zao kwa wino wa dhahabu.

WALHAMDULILLAHI RABBIL ALAMIN.

SAYYID ABUL A'LA MAUDUDI.

FAHARISI YA SURA

Sura		Ukurasa
1.	AL-FATIHAH	1
2.	AL-BAQARAH	5
3.	AALI-IMRAN	69
4.	AN-NISAA	102
5.	AL-MAIDAH	143
6.	AL-AN-AM	170
7.	AL-AARAF	199
8.	AL-ANFAL	235
9.	AT-TAWBA	250
10.	YUNUS	272
11.	HUD	290
12.	YUSUF	309
13.	AR-RAAD	325
14.	IBRAHIM	332
15.	AL-HIJR	339
16.	AN-NAHL	348
17.	BANI ISRAIL	364
18.	AL-KAHF	379
19.	MARYAM	394
20.	TA HA	403
21.	AL-ANBIYAA	415
22.	AL-HAJJ	426
23.	AL-MUUMINUN	436
24.	AN-NUR	446
25.	AL-FURQAN	456
26.	ASH-SHUARAA	464
27.	AN-NAML	478
28.	AL-QASAS	488
29.	AL-ANKABUUT	498
30.	AR-RUM	506
31.	LUQMAN	513
32.	AS-SAJDAH	518
33.	AL-AHZAB	522
34.	SABA	538
35.	FATIR	545
36.	YASYN	551
37.	AS-SAAFFAT	558
38.	SAD	570
39.	AZ-ZUMAR	578
40.	AL-MUUMIN	587
41.	HA-MYM-SAJDAH	597
42.	ASH-SHUURA	603
43.	AZ-ZUKHRUF	610
44.	AD-DUKHAN	618

Sura		*Ukurasa*
45.	AL-JATHIYAH	623
46.	AL-AHQAF	628
47.	MUHAMMAD	633
48.	AL-FAT-H	638
49.	AL-HUJURAT	644
50.	QAF	648
51.	ADH-DHAARIYAT	652
52.	AT-TUR	656
53.	AN-NAJM	660
54.	AL-QAMAR	665
55.	AR-RAHMAN	669
56.	AL-WAQIAH	674
57.	AL-HADYD	680
58.	AL-MUJADILAH	685
59.	AL-HASHR	689
60.	AL-MUMTAHINAH	693
61.	AS-SAFF	696
62.	AL-JUMUA	698
63.	AL-MUNAAFIQUN	701
64.	AT-TAGHAABUN	703
65.	AT-TALAQ	706
66.	AT-TAHRYM	709
67.	AL-MULK	712
68.	AL-QALAM	715
69.	AL-HAQQAH	719
70.	AL-MA'ARIJ	722
71.	NUH	725
72.	AL-JINN	728
73.	AL-MUZZAMMIL	731
74.	AL-MUDDATHTHIR	733
75.	AL-QIYAMA	737
76.	AD-DAHR	740
77.	AL-MURSALAT	743
78.	AN-NABAA	746
79.	AN-NAZIAT	749
80.	ABASA	752
81.	AT-TAKWYR	755
82.	AL-INFITAR	758
83.	AL-MUTAFFIFYN	760
84.	AL-INSHIQAQ	763
85.	AL-BURUJ	765
86.	AT-TARIQ	768
87.	AL-A'LAA	770
88.	AL-GHASHIYAH	772
89.	AL-FAJR	774
90.	AL-BALAD	777
91.	ASH-SHAMS	779

92.	AL-LAYL	781
93.	ADH-DHUHAA	783
94.	ALAM-NASHRAH	785
95.	AT-TYN	786
96.	AL-ALAQ	787
97.	AL-QADR	789
98.	AL-BAYYINAH	790
99.	AZ-ZILZAL	792
100.	AL-AADIYAT	793
101.	AL-QARIAH	794
102.	AT-TAKAATHUR	795
103.	AL-ASR	796
104.	AL-HUMAZAH	797
105.	AL-FYL	798
106.	QURAYSH	799
107.	AL-MAUN	800
108.	AL-KAWTHAR	801
109.	AL-KAFIRUN	802
110.	AN-NASR	803
111.	AL-LAHAB	804
112.	AL-IKHLAS	805
113.	AL-FALAQ	806
114.	AN-NAAS	807

FAHARISI YA JUZUU

			Ukurasa
JUZUU	1	ALIF LAM MYM	1
JUZUU	2	SAYAQULU	31
JUZUU	3	TILKAR RUSULU	59
JUZUU	4	LAN TANALU	84
JUZUU	5	WALMUHSANAT	109
JUZUU	6	LA YUHIBB	137
JUZUU	7	WA IDHASAMIUU	162
JUZUU	8	WALAW ANNANA	185
JUZUU	9	QAALAL MALAU	213
JUZUU	10	WAALAMUU	242
JUZUU	11	YAATADHIRUN	265
JUZUU	12	WAMAA MIN DAABBA	290
JUZUU	13	WAMAA UBARRIU	317
JUZUU	14	RUBAMAA	339
JUZUU	15	SUBHANA	364
JUZUU	16	QALA ALAM	390
JUZUU	17	IQTARABA	415
JUZUU	18	QAD AFLAHA	436
JUZUU	19	WA QALA	458
JUZUU	20	AMMAN KHALAQ	484
JUZUU	21	UTLU MAA	503
JUZUU	22	WAMAN YAQNUT	527
JUZUU	23	WAMAA LIYA	553
JUZUU	24	FAMAN ADHLAMU	582
JUZUU	25	ILAYHI YURADDU	602
JUZUU	26	HAA MYM	628
JUZUU	27	QALA FAMAA KHATBUKUM	654
JUZUU	28	QAD SAMIA	685
JUZUU	29	TABARAKA	712
JUZUU	30	AMMA	746